29 OKTOBA, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Tatu – Tarehe 29 Oktoba, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, karibuni katika Mkutano wetu wa Tano, Kikao cha Tatu.

Swali la kwanza litaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Sasa ninamwita Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mbunge wa Singida Mjini, aulize swali lake.

Na. 36

Ukarabati na Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Singida

MHE. YAGI M. KIARATU aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati na kujenga upya Hospitali ya Manispaa ya Singida?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali Kongwe Nchini. Aidha, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi Mwaka 2025/2026 jumla ya shilingi bilioni 62.28 zimetolewa, kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe 58. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Mwaka 2023/2024 Hospitali ya Manispaa ya Singida imepokea jumla ya shilingi bilioni moja, kwa ajili ya ukarabati wa jengo la upasuaji, ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura *(EMD),* na jengo la wazazi lenye chumba cha upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Hospitali ya Manispaa ya Singida imetengewa jumla ya shilingi milioni 800, kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa majengo yaliyosalia. Serikali itaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe kisha kuendelea na vituo vya afya na zahanati kongwe, kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya ngazi ya msingi. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, swali la nyongeza!

MHE. YAGI M. KIARATU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kuboresha huduma za afya; na moja ya eneo ni Hospitali ya Manispaa ya Singida. Manispaa ya Singida ilikuwa haina hospitali ya wilaya kwa muda mrefu sana, na niishukuru Wizara kwa kukubali kuachia majengo yaliyokuwa hospitali ya mkoa, kuwa hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia inatueleza kwamba, majengo hayo yana zaidi ya miaka 70, kwa maana hiyo ni chakavu sana. Kama alivyosema Naibu Waziri hapo, majengo mazuri ni matatu tu, kwa maana ya jengo la mama na mtoto, jengo la dharura, na hiyo *theatre* iliyokarabatiwa, mengine yote hayafai, na bahati nzuri mwenyewe alikuja na akajionea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, kwa hadhi ya hospitali ya wilaya na majengo yaliyoko hapo, naiomba sana Serikali ifanye utaratibu wa kujenga upya, na yeye mwenyewe ni shahidi. Sasa kwa namna alivyoona, ninaomba majibu ya Serikali kwa hadhi ya hospitali ya wilaya ile, haifai kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hiyo ni kama imeanza upya, hakuna majengo mazuri...

MWENYEKITI: Swali, Mheshimiwa!

MHE. YAGI M. KIARATU: ...hakuna vifaa tiba, lakini hakuna madaktari bingwa! Ninaomba Waziri atoe *commitment* ya Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana dada yangu, Mheshimiwa Kiaratu. Ni kweli tumefanya ziara wote pamoja katika hospitali yetu ile, na shilingi bilioni moja, ambayo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iliitenga kwa awamu ya kwanza; tumetembelea majengo, ambayo yamekamilika, majengo bora, na yanatoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge; kwa hii shilingi milioni 800, ambayo tumeitenga, sasa iende ikafanye kazi kwenye maeneo ambayo yamesalia. Tutaendelea na ujenzi kwa awamu kulingana na mahitaji, ili kuhakikisha kwamba, hospitali yetu hii imeenda kutoa huduma bora ambazo zinatakiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kutenga fedha, ili kuhakikisha kuwa, maeneo yale nyeti na muhimu kabisa, ambayo ameyaainisha, na bajeti hii inafuatia ile ziara ambayo tulifanya pamoja kwenye hospitali yetu, ili kuendelea kukamilisha miundombinu hii. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali la nyongeza!

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Afya vya Tawa, pamoja na Dutumi, ni vituo vikongwe na vichakavu sana. Mheshimiwa Naibu Waziri aliniahidi kuwa, baada ya bajeti kupita ukarabati utaanza mara moja. Sasa tayari robo ya mwanzo ya bajeti imepita, na pale hakuna dalili za kuanza kwa ukarabati. Je, ni lini sasa ukarabati katika vituo hivi vya afya utaanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakiri kwamba, ni kweli Mheshimiwa Mfaume ameleta ombi hili na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI tumelipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vikao vya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tumepitia andiko upya, ili kuthibitisha vile vituo vikongwe vyote nchini. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuko hatua za mwisho za kupitisha vituo hivyo; kuna vile vichache ambavyo vilikuwa vimesahaulika, navyo vitajumuishwa kwenye vituo hivyo vikongwe, ili tuanze kuvitengea bajeti, na fedha ianze kushuka kule kwenye vituo vyetu hivi vikongwe vya afya. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abdallah Chikota!

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaishukuru Serikali kwa kupeleka fedha Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa hospitali yetu ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ile ina changamoto kubwa sana ya *walk ways* kati ya jengo moja hadi lingine. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Chikota; tulikuwanaye kwenye uzinduzi wa bima ya afya kwa wote, awamu ya pili. Wananchi walijitokeza sana kwenye mkutano ule kwa sababu, yeye pia, ni Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, Serikali imeendelea kutenga fedha, kwa ajili ya ukarabati na umaliziaji wa hospitali; kuna zile kongwe, lakini kuna hizi mpya, ambazo tumeendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba, tunakamilisha miundombinu hii, hasa kwenye upande wa ujenzi wa uzio na *walk ways*. Tunakumbuka Mwaka 2025/2026 jumla ya hospitali 48 zimetengewa bajeti ya shilingi bilioni 32.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Chikota, pamoja na wananchi wa jimbo analotoka kwamba, tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha tunakamilisha miundombinu hii, ili wananchi wapate huduma ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anataka kuhakikisha hospitali hizi zinatoa huduma stahiki kwa wananchi wetu. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Johannes Lukumay, swali la nyongeza!

MHE. JOHANNES L. LUKUMAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Serikali:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kupeleka shilingi milioni 500, kwa ajili ya kujenga jengo la *maternity complex* katika Hospitali ya Wilaya ya Arumeru ya Olrumet, iliyoko katika Jimbo la Arumeru Magharibi. Si hiyo tu, uwekezaji mkubwa katika nchi hii umefanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan; kwa mfano, kwenye Hospitali ya Olrumet kuna *digital x-ray,* na *digital ultra sound*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, nisipoteze muda. Ninapenda kufahamu; Je, Serikali itajenga lini jengo ya magonjwa ya dharura au jengo la dharura *(EMD)* katika Hospitali ya Wilaya ya Olrumet?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa *Doctor* Lukumay. Tumefanya ziara katika jimbo lake tukiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ajili ya uzinduzi wa majengo mbalimbali katika kituo cha afya, ambacho amekitaja:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa *Doctor* Lukumay, huduma ya *EMD* inaendelea kutolewa katika hospitali yetu ya wilaya. Kwa suala la kuweka jengo rasmi; namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutampa ushirikiano wa dhati katika kuhakikisha tunakamilisha ujenzi wa hili jengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha hospitali zote za wilaya zinakuwa na huduma zote, na kwamba zinatoa zaidi ya zile huduma 12 kwa wananchi wetu. Namhakikikishia Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wananchi anaowaongoza kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, nyakati

zote tutaendelea kuwapa ushirikiano kuhakikisha tunakamilisha haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yale ambayo ameshukuru, na ametoa ushuhudu hapa; Serikali ina dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba, hospitali hizi zinakamilika na tunahamia sasa kwenye ukamilishaji tu wa vituo vya afya na zahanati. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Baraka, swali la nyongeza!

MHE. ASHA R. BARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri; ni lini Serikali itaongeza kituo cha afya Wilaya ya Uvinza, hasa kata za Nguruka, Mtego wa Noti, pamoja na Mganza? Tangu mimi ninasoma, kituo cha afya ni kimoja hichohicho, hadi nimekuwa na umri huu nilionao!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninataka kujua. Je, ni lini Serikali itaongeza hicho kituo cha afya, pamoja na wodi za kina mama, na kadhalika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nampongeza Mheshimiwa Asha Baraka, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Dar es Salaam, lakini kwa sababu anawasemea akinamama, mpaka wale wa Uvinza, na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI tumeendelea kuainisha maeneo yote yenye changamoto ya vituo vya afya, hasa vile vya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Asha Baraka kwamba, kupitia swali ambalo ameliuliza Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, tutachukulia maanani

swali lako na kuhakikisha kwamba, eneo hili tunalitengea bajeti, na kuanza ujenzi wa kituo cha afya. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, nami niulize swali dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Bunda Mjini kinatoa huduma kwa watu wengi sana mpaka wilaya za jirani katika Mkoa wa Mara; lakini pale kuna upungufu wa *OPD,* wodi ya kina mama, na ya kina baba. Juzi nimetoka jimboni, nimefanya kikao na wauguzi wa pale, hilo ndilo hitaji lao kubwa, wanaelemewe. Je, ni lini, sasa watatuletea fedha, zaidi ya shilingi milioni 700, tuweze kukamilisha ujenzi wa majengo hayo, ili wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini waweze kupata huduma stahiki za afya?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ambavyo ameliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali Mheshimiwa Mbunge alikuja na ombi maalum kabisa la Kituo cha Afya cha Manyamanyama. Tayari tumekitengea fedha, kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu, ambayo Mheshimiwa Mbunge ameiwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuondoa hofu Mheshimiwa Mbunge; kwa eneo hili la Bunda Mjini, na kwa kuwa ana hospitali pale ya wilaya, tutaendelea kutenga fedha, ili kuhakikisha kituo hiki nacho tunakitengea fedha kukamilisha miundombinu, ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja, ili kukata zile *referral* za kutoka kwenye kituo cha afya kwenda kwenye hospitali ya wilaya ziende zile zilizo za lazima tu, lakini wananchi wengine watibiwe kwenye Kituo cha Afya cha Bunda Mjini, waweze kurejea nyumbani, warejee majukumu yao. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi, swali la nyongeza.

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami namuuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Katoro tuna Kata ya Magenge na Kata ya Kaseme. Wananchi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wanakuja kutibiwa katika Kituo cha Afya cha Katoro ambacho kiko mbali sana kutoka kwao. Je, ni lini Serikali itatenga fedha, ili kuwajengea kituo cha afya katika Kata za Kaseme na Kata ya Katoro, ili wananchi hawa wasipate usumbufu wa safari ndefu ya kwenda katika Mji wa Katoro kupata huduma ya afya? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi, Mbunge wa Jimbo la Katoro, kwa namna ambavyo anafuatilia maendeleo, pamoja na huduma za afya, siyo tu katika jimbo lake, bali hata katika majimbo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi kwamba, tutaendelea kutenga fedha, na kuainisha vituo hivi na kuangalia mahitaji, kulingana na idadi ya watu. Kwa sababu, Jimbo la Katoro ni miongoni mwa majimbo yenye idadi kubwa ya wananchi, ndiyo maana tumekuwa tunakamilisha katika hospitali yake ile ya wilaya. Pia, kuna ujenzi wa *emergency* kubwa katika *trunk road* ile, lakini pia, kuna ujenzi mkubwa unaenda kukamilika Mwezi Januari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ushirikiano ambao tunaendelea kumpatia kwenye eneo la vituo vya afya, hivyo ambavyo ameviainisha, tutaendelea kuainisha na kuangalia mahitaji, na kuhakikisha tunatenga bajeti, kwa ajili ya kujenga vituo hivi. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge wa Kigamboni, aulize swali lake.

Na. 37

Kuifanya Dar es Salaam Kuwa *Metropolitan Authority*

MHE. KAKULU B. KAKULU K.n.y. MHE. HARAN N. SANGA aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuifanya Dar es Salaam kuwa, *Metropolitan Authority,* ili kuiwezesha kuimarisha sheria na taratibu za mamlaka hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kasi ya ukuaji wa Jiji la Dar es salaam, na kwa lengo la kuboresha utendaji kazi, utoaji wa huduma kwa wananchi, na kuimarisha uhusiano kati ya Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam na taasisi nyingine za kimkoa, Kitaifa, na Kimataifa, Serikali inatazama uwezekano kuanzisha Mamlaka ya Dar es Salaam *Metropolitan (Dar es Salaam Metropolitan Authority)*. Serikali imefanyia kazi mapendekezo ya maboresho ya Muundo wa Jiji la Dar es Salaam kuwa, Mamlaka ya Dar es salaam Metropolitan, ambayo itahusika na shughuli za uratibu wa masuala mtambuka yanayovuka mipaka ya manispaa zaidi ya moja. Aidha, mapendekezo haya yamezingatia uzoefu wa nchi nyingine na mifumo ya kisheria iliyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuwa, Mamlaka ya Dar es salaam *Metropolitan* yako katika hatua mbalimbali za mapitio na tathmini. Kwa muktadha huu, iwapo mapendekezo haya yataridhiwa, taratibu mbalimbali zitachuliwa, ili kuweza kukamilisha mpago huu. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haran Sanga, swali la nyongeza!

MHE. KAKULU B. KAKULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu na kasi ya ukuaji wa mji wa Dar es Salaam, na kweli makadirio ya ukuaji wa watu ifikapo 2030 tunatarajia kuwa na watu karibu milioni 10. Kwa umuhimu wa Jiji la Dar es Salaam, na kwa umuhimu wa shughuli mtambuka ambazo zina-*cut across* halmashauri zote; Je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha jambo, ili lifanyike mapema iwezekanavyo, kwa ajili ya kurahisisha huduma kwa wananchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mbagala kwa namna ambavyo anafanya kazi kubwa na nzuri ya kuwasemea Wananchi wa jimbo lake na Wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam, na Watanzania kwa ujumla:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, idadi ya wananchi katika Mkoa wa Dar es Salaam imeendelea kuongezeka siku hadi siku. Kwa mujibu wa *projections* za Benki ya Dunia *(World Bank Population Growth Services)* ni kweli kwamba, tunatarajia ifikapo 2030 idadi ya wananchi katika Mkoa wa Dar es Salaam itakuwa zaidi ya milioni 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, huu ni mkoa ambao una shughuli nyingi na kubwa za kiuchumi za kijamii, hivyo unaingiliana sana na usafiri kati ya manispaa moja na nyingine, ukilinganisha na mikoa mingine kote nchini; ni Mkoa ambao ni kitovu cha biashara, ni kioo cha nchi yetu. Serikali inatambua umuhimu wa kulifanya Jiji la Dar es Salaam, au Mkoa wa Dar es Salaam kuwa, mkoa wa kisasa zaidi na kuweza kuhakikisha kwamba, tunaboresha taratibu za uongozi wa mkoa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Serikali imeanza kuchukua hatua. Kwanza, tumefanya maandiko ya kujiridhisha namna nzuri ya kuwa na Dar es Salaam *Metropolitan Authority,* na tumefanya *consultation* kwa kampuni moja ya Ufaransa inayoitwa *Esperia Company Limited,* ambayo inashirikiana na kampuni ya Tanzania inayoitwa *Dentos Company Limited.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tuna maandiko mawili; tunalo andiko ambalo limekuwa *proposed* na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, na vilevile tunalo andiko ambalo *consultants* hawa nao wameliandika. Kazi inayoendelea sasa ni ku-*harmonize* maandiko haya yote mawili, ili tupate andiko moja bora, ambalo litatumika kwenye mfumo zaidi wa kuunda mamlaka hii ya Dar es Salaam kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali italifanyia kazi, na mara taratibu hizi zikikamilika, basi tutakwenda hatua nyingine; lengo ni kuboresha Jiji letu la Dar es Salaam. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sara Msafiri, swali la nyongeza!

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, naipongeza Serikali, imekuwa ikitoa fedha nyingi kupitia programu za kuboresha majiji, kama programu za *TACTIC* na *DMDP*. Wamekuwa wakijenga masoko mazuri, stendi nzuri, na miundombinu ya barabara kwenye majiji makubwa, lakini kupitia halmashauri zetu tumekuwa na changamoto sana ya barabara, masoko, na stendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, lini Serikali italeta programu maalumu, kwa ajili ya kuboresha miundombinu kwenye halmashauri zetu na kwenye miji midogo, kama ilivyo Mji wa Turiani, Mvomero?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, namshukuru sana Mheshimiwa Sara Msafiri. Nampongeza kwa kazi kubwa anayoifanya kuwasemea Wananchi wa Jimbo la Mvomero, lakini tu namhakikishia kwamba, Serikali imeendelea katika kila mwaka wa fedha kuongeza bajeti, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara katika halmashauri zetu, masoko, na vituo vya mabasi (stendi), pamoja na *parking* za malori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya hivyo, kwanza kwa dhamira ya kuboresha miji na halmashauri zetu, lakini pili; tunafanya hivyo kama sehemu ya kusogeza huduma bora za kijamii, na pia, kupata vyanzo vya mapato katika halmashauri zetu. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti, kwa mfano ya mwaka huu 2026/2027; Serikali imetoa maelekezo ya kutenga angalau asilimia tano katika vyanzo vya mapato ya ndani ya halmashauri visivyolindwa, kwa ajili ya ujenzi wa masoko, na shughuli hizi zimeanza. Ukipita pale Dar es Salaam, Manispaa ya Ubungo, Kinondoni, Temeke, na baadhi ya majiji na manispaa, Serikali imeendelea kujenga vibanda, kwa ajili ya wafanyabiashara wadogowadogo kutokana na ile asilimia tano ya vyanzo vya mapato visivyolindwa, lakini tunayo maandiko ya kimkakati ya kujenga stendi na masoko kote nchini yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kufanya hivyo. Tunawakaribisha Halmashauri ya Mvomero pia, kutumia fursa hiyo ya kuwasilisha maandiko, kutenga fedha za mapato ya ndani,

lakini pia, Serikali Kuu kuona uwezekano wa kujenga maeneo yale ambayo yana umuhimu wa kuwa na miundombinu kama hiyo. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, aulize swali lake.

Na. 38

Hitaji la Shule ya Msingi, Kijiji cha Mheza, Same Mashariki

MHE. ANNE K. MALECELA aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Shule ya Msingi Kitongoji cha Igoma, Kata ya Maore, katika Kijiji cha Mheza ambacho kipo jirani na Mbuga ya Mkomazi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza mipango ya ujenzi wa shule za msingi katika vijiji na vitongoji vyenye sifa stahiki, ili kuwezesha wanafunzi kupata huduma ya elimu kwa ukaribu na usalama. Kitongoji cha Igoma, Kijiji cha Mheza, Kata ya Maore katika Halmashauri ya Wilaya ya Same, kina jumla ya wananchi 924 na kipo jirani na Mbuga ya Mkomazi. Aidha, wanafunzi wa kitongoji hicho wanasoma katika Shule ya Msingi Njiro, iliyopo umbali wa kilometa sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitongoji cha Igoma, Kata ya Maore, kina kituo shikizi kimoja chenye madarasa mawili, ambayo

yanatumika na wanafunzi 26 wa darasa la awali na la kwanza. Halmashauri imetenga eneo la ekari saba, kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi, ambapo katika mwaka wa fedha 2026/2027, shilingi milioni 12 za mapato ya ndani ya halmashauri zimetengwa, kwa ajili ya ujenzi wa matundu sita ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umbali wa kitongoji hicho kwenda Shule ya Msingi Njiro, na kwa kuzingatia mazingira hatarishi ya Mbuga ya Mkomazi, Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti zijazo za ujenzi wa miundombinu ya shule shikizi, ili iweze kujengwa katika Kitongoji cha Igoma, Kata ya Maore. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza!

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nasema ukweli, nimeyapenda majibu ya Serikali. Wananchi wa Kitongoji hiki cha Igoma, ni kweli wanaishi kwenye *isolation,* lakini si kwamba, wametaka, kule wamefuata ardhi, ili waweze kulima. Sasa ninaomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekiri kwamba, Wananchi wa Igoma wana matatizo matatu zaidi yanayowafanya watoto washindwe kwenda shule; kwanza, ni hali hatarishi, pili umbali, na kadhalika. Nasema ukweli, mimi ninaishi Halmashauri ya Wilaya ya Same; hawana mpango wa kujenga shule ya msingi kwenye Kitongoji hiki cha Igoma.

Je, Serikali, hamuoni ni vyema mkalichukua hili jambo *serious* kwa sababu, watoto wale wanakosa haki yao ya kupata elimu, mkajenga shule ya msingi Kijiji cha Igoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasitegemee Halmashauri ya Wilaya ya Same na ninaomba kwa unyenyekevu. Ninaomba shule ya msingi Kijiji cha Igoma, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nampongeze sana mama yangu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, amekuwa msemaji na mwakilishi madhubuti sana kwa Wananchi wa Jimbo la Same Mashariki. Mimi nimeshafanya ziaranaye mara kadhaa katika jimbo lile, nikajionea moto wake, na wananchi ambavyo wanamuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunafahamu Kitongoji cha Igoma kiko katika eneo hatarishi, kinahitaji kuwa na shule ya msingi, ili kuweza kuokoa maisha ya watoto wanaotembea umbali wa zaidi ya kilomita sita; kwenda, sita, kurudi 12 na ni watoto wadogo! Tumekubaliana kwa sababu, ndio tumelipokea Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana na Halmashauri ya Wilaya ya Same. Sisi Serikali kuu tutaona uwezekano wa kutenga fedha na kuanza ujenzi wa madarasa mengine, ili watoto wanapokwenda darasa la tatu wapate darasa; darasa la nne wapate darasa; mpaka tunamaliza darasa la saba, ili kuhakikisha watoto wetu wawe wanasoma katika mazingira salama na bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge suala hilo tumelichukua, na tuko *serious*-nalo. Tutakwenda kulifanyia kazi kwa manufaa ya wananchi wa eneo la Igoma. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chacha Wambura, swali la nyongeza.

MHE. CHACHA M. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Geita ni mojawapo ya miji ambayo inakua kwa kasi na watu wake ni wengi; tunajitahidi, tuna watoto wa kutosha! Katika ukuaji huu wa Mji wa

Geita, tumeshuhudia shule sasa zinazidiwa; ukienda katika Kata ya Nyankumbu, eneo la Nyantorotoro A na Nyantorotoro B, kuna eneo la Shule ya Msingi Nyantorotoro lina wanafunzi zaidi ya 3,000 kwa shule moja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kufahamu kauli ya Serikali; ina mpango gani kuhakikisha kwamba, tunaongeza shule pale, ikizingatiwa wananchi wamepata eneo, wamenunua, eneo lipo. Sasa *commitment* ya Serikali kuongeza shule pale, ili watoto waweze kuwa kwenye uwiano mzuri, ni ipi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nampongeza Mheshimiwa Chacha Wambura, Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, namthibitishia kwamba, Serikali tunatambua katika shule zetu tumeweka *standard* ya idadi ya wanafunzi inayokubalika, katika shule, ili kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji kwa watoto. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kulisemea suala la eneo hili la Nyantorotoro, ambapo shule hii ina wanafunzi zaidi ya 3,000, na tunafahamu kwamba, shule ikiwa na wanafunzi zaidi ya 3,000 ni changamoto kwa walimu kuwa-*manage* vizuri, lakini pia, hata wanafunzi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie kwamba, tutakwenda kufanya tathmini kuona namna ambavyo tutaanza kutenga fedha, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa shule nyingine katika eneo hilo. Pia, nampongeza Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Geita Mjini kwa kutenga eneo hilo tayari kwa ujenzi wa shule. Kwa hiyo, hatua ya kwanza tumekwenda, tunakwenda hatua ya pili, kwa maana ya kutenga fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatenga fedha kwa awamu; mapato ya ndani, au fedha kutoka Serikali kuu kuhakikisha

kwamba, shule hiyo inajengwa, na wanafunzi wanapata mazingira bora ya kusomea. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, kuuliza swali dogo la nyongeza. Ninaipongeza sana Serikali kwa kujenga shule za sekondari nzuri sana, na za kisasa, lakini baadhi ya shule hizo zina changamoto za mabwalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kyela, Shule ya Sekondari ya KCM, Bondeni, na Ipande Mashariki, hazina mabwalo kabisa. Wilaya ya Rungwe, Shule ya Sekondari, ambayo ni kongwe sana; Rungwe Sekondari ina bwalo dogo na wanafunzi wamekuwa ni wengi. Kayuke Sekondari, Tukuyu Sekondari, Kisondela, Lupoto, na Bujinga, hakuna mabwalo kabisa. Sasa je, ni lini Serikali itaweka uzito wa kujenga mabwalo hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya, Mheshimiwa Fyandomo, kwa hoja hii muhimu. Ninaomba nimthibitishie kwamba, Serikali imeendelea kujenga mabwalo katika shule zetu, na zoezi hili ni endelevu. Katika kila mwaka wa bajeti, Serikali imekuwa inatenga fedha, kwa ajili ya ujenzi wa mabwalo katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba, katika miaka mitano ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kipindi ambacho tumejenga mabwalo mengi sana katika halmashauri zetu. Tunatambua kwamba, pamoja na ujenzi huo bado kuna uhitaji mkubwa wa ujenzi wa mabwalo katika shule nyingi, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, ikiwemo KCM, Ipande Mashariki, Rungwe, Kisondela, na nyingine zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, zoezi hili ni endelevu. Tutaendelea kuzitambua shule zote ambazo hazina mabwalo na tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kwenye bajeti zetu kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, lakini pia, kupitia Serikali Kuu, ili kuhakikisha tunajenga mabwalo katika shule hizo na wanafunzi wetu wanapata huduma bora. Naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ibrahim Shayo, swali la nyongeza!

MHE. IBRAHIM M. SHAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina halmashauri na manispaa ambazo ardhi yake ni finyu sana, hususan Moshi Mjini. Moshi Mjini, ardhi yetu sasahivi inaendelea kuisha. Nini Kauli ya Serikali kujenga shule za ghorofa, kuepukana na shule za majengo ya chini, ili kuhakikisha kwamba, tunatumia ardhi vizuri?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nampongeza sana Mheshimiwa Ibrahim Shayo, Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, kwa kazi kubwa anayoifanya kuwasemea wananchi wa Jimbo la Moshi na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, jana nimejibu swali hapa la Mheshimiwa Mama Mariam Kisangi, kuhusiana na ujenzi wa mabweni na majengo mengine katika Shule ya Sekondari ya Kibasila kwa mfumo wa maghorofa. Ninaomba nikuhakikishie tu kwamba, Serikali tumeanza katika miji yote, majiji, na manispaa, yale ambayo yana ardhi finyu. Tumetoa maelekezo na mwongozo kwa halmashauri kufanya tathmini ya maeneo husika, na kuweza ku-*customize* ramani za maghorofa katika maeneo hayo, ili tuweze kutumia vizuri ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nikuthibitishie tu kwamba, suala hilo tayari tumetoa mwongozo madhubuti kabisa na unatekelezwa kote nchini na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi itumie fursa hiyo. Ikiwa kuna eneo wanahitaji ujenzi wa majengo ya ghorofa, wapendekeze, walete michoro; itapitiwa na *directorate* yetu ya *infrastructure* na baadaye tutawapa kibali. Serikali itaendelea kushirikiananao kuhakikisha kwamba, tunajenga majengo ya kwenda juu badala ya kujenga majengo ya msambao, ambayo yanatumia ardhi kubwa zaidi. Naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge nitakaowapa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, naomba muulize kwa kifupi kwa sababu, mko wengi. Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba pia, ujibu kwa kifupi!

Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza!

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Shule ya *Mulbadaw Primary* ni ya muda mrefu na imechakaa sana. Je, lini Serikali itaunga jitihada za halmashauri kuhakikisha shule hii tunaweza kuikarabati, ili isiweze kuleta madhara, hasa ukizingatia tahadhari za *El Nino* na jiografia ya Wilaya ya Hanang?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Jimbo la Hanang kwamba, tumefanya tathmini ya shule zote chakavu na tumeandaa andiko moja la kwenda Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Wizara ya Fedha, kwa ajili ya kujenga na kukarabati shule zote chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, nimwelekeze Mkurugenzi wa Hanang awasilishe andiko maalum la shule hiyo kwa sababu, umesema ni chakavu sana, haihimiliki, ili

tuweze kuona namna nzuri ya kupata fedha, kwa ajili ya kuifanyia matengenezo, watoto wasome katika mazingira salama. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paulo Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Mbulu ina shule 12 za sekondari za *A-level.* Hadi sasa, wanafunzi wa kidato cha tano na sita...

(Hapa kipaza sauti kilizimika)

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: …je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kujenga mabweni katika shule hizo za kidato cha tano na sita katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumeweka mpango wa ujenzi wa mabweni, na kipaumbele kikiwa kwenye shule za kidato cha tano na sita. Ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Issaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini kwamba, tutaendelea kutenga fedha kwenye bajeti zetu kuhakikisha shule hizo za kidato cha tano na sita zote 12, kwa sababu zina sifa za kujengewa mabweni, tutaendelea kwa awamu kuleta fedha kuhakikisha kwamba, tunajenga mabweni katika shule hizo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza!

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Shule ya Msingi Majalila iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika imezidiwa, ina idadi ya wanafunzi zaidi ya 2,000

wanaosoma. Ni lini Serikali itapeleka fedha za kuwasaidia kujenga shule nyingine mpya? Serikali ya kijiji imeanzisha, imejenga madarasa mawili; ninataka kupata ufafanuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Tanganyika. Namthibitishia tu kwamba, Serikali inatambua ziko shule zenye wanafunzi wengi, zaidi ya kiwango ambacho kinakubalika. Nawapongeza kwa kuanza; kwanza, kwa kupata eneo la ujenzi, lakini pili, na kwa kuanza hatua za awali za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza wananchi, wewe Mheshimiwa Mbunge, na *management* yote ya Halmashauri ya Tanganyika. Ninaomba nikuthibitishie tu kwamba, Serikali tumelichukua hilo, tutalifanyia kazi, ili katika bajeti zetu tutoe kipaumbele, kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Juma Mustafa, swali la nyongeza!

MHE. JUMA M. KAWAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii niulize swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igalula ni jimbo ambalo asilimia kubwa linapatikana mazingira ya vijijini. Kwanza, ninapenda niwapongeze Wananchi wa Jimbo la Igalula, kwa kushirikiana na Serikali, kwa kujenga maboma mengi ya shule za msingi, ambayo bado hayajaanza kutumika. Je, ni lini Serikali itatuletea fedha, kwa ajili ya kumalizia maboma haya, ili watoto waweze kuyatumia, kwa ajili ya kusoma, kama vile wanavyoyatumia watoto wengine hapa nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa

Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Mustafa, Mbunge wa Jimbo la Igalula, ninampongeza kwa kazi nzuri. Ninaomba nimthibitishie tu kwamba, bahati njema Serikali tumefanya sensa ya maboma yote kote nchini tukayatambua, na gharama ya fedha inayohitajika, kwa ajili ya kukamilisha maboma yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Jimbo la Igalula, tunayo idadi ya maboma yote, ambayo yamejengwa, kwa ajili ya ukamilishaji, na tumeendelea kufanya hivyo. Katika mwaka huu wa fedha tayari kuna fedha zimepelekwa katika baadhi ya halmashauri zetu na zoezi linaendelea; zikiwemo za ukamilishaji wa maboma, lakini pia, za ukarabati wa shule kongwe na chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, safari ni hatua, tutawapa kipaumbele Igalula kuhakikisha kwamba, maboma hayo pia, yanapata fedha, kwa ajili ya kukamilisha madarasa hayo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Emmanuel Khambay, swali la nyongeza!

MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, na mimi, niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itajenga shule ya msingi katika Kitongoji cha Misuna na Mkalama, Kijiji cha Kiongozi, kutokana na changamoto wanayopata watoto kwenda umbali mrefu katika Shule ya Msingi Kiongozi na Shule ya Msingi Kiru?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini, Mheshimiwa Emmanuel Khambay na ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunafanya tathmini ya vitongoji vyenye idadi kubwa ya wananchi,

na wanafunzi ambao wanatembea umbali mrefu kwenda kwenye shule za jirani ambazo wanasoma, shule mama, ili tuendelee kujenga shule shikizi, lakini baadaye ziweze kupata sifa ya kuwa shule kamili za msingi. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, tutafanyia tathmini kitongoji hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Babati, waweze kutuletea tathmini ya vigezo vya kitongoji hicho, na mpango wa halmashauri. Sisi Serikali Kuu tuone namna nzuri ya kupeleka huduma hiyo muhimu kwa wanafunzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda, swali la nyongeza!

MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Nina swali dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vijiji vya Likwaya kuna upungufu mkubwa, hakuna shule kabisa, lakini wananchi wamejenga shule yao ndogo na madarasa mawili, na wana eneo kubwa kabisa wamelitenga. Je, nini Kauli ya Serikali kuhakikisha wanapeleka fedha kukamilisha shule hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Kauli ya Serikali; kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Yahya Ismael Nawanda, Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, kwa kazi nzuri na kubwa sana anayoifanya. Nina-*declare interest* kwamba, Mheshimiwa Yahya Nawanda alikuwa *DC* wangu wa Lindi, nikiwa Mganga Mkuu wa Manispaa ya Lindi. Ninajua uchapakazi wake, ni kiongozi madhubuti sana kwa hiyo, ninakupongeza na sisi tutaendelea kukuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza yeye na Wananchi wa Kijiji cha Likwaya kwa kuandaa eneo la ujenzi wa

shule ya msingi na kuanza ujenzi huo. Namthibitishia tu kwamba, Serikali tumelichukua hilo kwa uzito wake, na tutafanya taratibu za kibajeti kwa awamu kuhakikisha kwamba, watoto hao katika kijiji hicho wanapata shule. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri – TAMISEMI, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Jafari Rajab, tunawashukuru sana kwa majibu yenu kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Sasa ninamwita Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, aweze kuuliza swali lake.

Na. 39

Kuwaunganisha Wananchi wa Kaya Maskini na Fursa Nyingine

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kuunganisha kaya maskini na fursa nyingine za kujikwamua na umaskini, badala ya kutegemea uwezeshaji mdogo wa *TASAF*?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuwawezesha wananchi na kaya masikini, ili kujiondoa katika umasikini kwa kuwaunganisha na fursa mbalimbali za kiuchumi badala ya kutegemea uwezeshaji wa *TASAF* pekee. Fursa hizo ni pamoja na kuwapatia elimu ya ujasiriamali, stadi za kazi, uanzishaji wa vikundi

vya kuweka akiba, pamoja na kuwaunganisha na taasisi za kifedha, kwa ajili ya kuwawezesha kupata mikopo ya ujasiriamali, ili kuongeza kipato na kujenga uwezo wa kujitegemea. Aidha, vijana kutoka kaya maskini wanaochaguliwa kujiunga na elimu ya juu, wameunganishwa na mfumo wa mikopo ya elimu ya juu, ili kuwawezesha kupata mikopo ya elimu ya juu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza!

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri, na mpango wa *TASAF* ni mzuri sana. Tumeona namna ambavyo umesaidia baadhi ya wananchi na miradi ya maji pia, elimu na afya, na hasa huu mpango wa vijana wanaoenda chuo kikuu, wanaotokea katika *TASAF,* kuunganishwa na mfumo wa elimu ya juu. Sasa tunajua awamu zilizopita zimeisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza ni kwamba, je, ni lini Serikali, sasa, itaanza mpango wa awamu ya tatu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Katika mikutano yangu mingi ya hadhara, kila mkutano ninapata mwananchi, ambaye analalamikia kuachwa kwenye *TASAF*.

Je, Serikali ina mpango gani sasa katika awamu ya tatu inayokuja, kuhakikisha kwamba, inaboresha ule upatikanaji wa wanufaika wa *TASAF,* ili kupunguza malalamiko ya wananchi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge Asenga, kwa namna ambavyo ameendelea kuwawakilisha vizuri Wananchi wake wa Kilombero. Mara zote tumeona namna anavyowatetea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asenga nikianza na swali lake la

kwanza, kuwa ni lini mpango huu wa awamu ya tatu utakwenda kuanza; Serikali ilikamilisha hatua zile muhimu za uanzishaji wa mpango wa awamu ya tatu ikiwa katika kusanifu mpango wenyewe, lakini kuandaa miongozo mbalimbali ya utendaji katika kutekeleza mpango huu wa awamu ya tatu. Pamoja na hayo, Serikali iko katika hatua ya utekelezaji wa kutambua mamlaka ambazo zitakuja kujumuishwa kwenye mpango huu wa *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesaini makubaliano na Benki ya Dunia, ambapo tayari Dola za Kimarekani 296 zimetengwa, ili kutekeleza mpango huu wa awamu ya tatu, na katika utekelezaji huo kaya 575,000 zitakwenda kunufaika. Kwa hiyo, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, tayari mpango huu hatua zote zimekamilika, na tayari sasa tunakwenda kuanza utekelezaji wa mpango wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili, utaratibu wa kuwapata walengwa; utaratibu wa kuwapata walengwa ni shirikishi. Jamii imekuwa ikishirikishwa kwa ujumla kupitia Viongozi wa Serikali za Mitaa na Viongozi wa Serikali ya Kijiji, maana wenyewe ndiyo wanaowafahamu walengwa haswa. Kwa hiyo, kwa ujumla mpango huu wa *TASAF* ni shirikishi, walengwa wamekuwa wakitambuliwa kwa kupitia jamii husika na kuwapa kipaumbele wale ambao wana umasikini uliokithiri. Kwa hiyo, kwa kuzingatia vigezo vile vya umasikini uliokithiri, walengwa hao wamekuwa wakiwekwa kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pale inapobainika kuwa, walengwa waliowekwa kwenye mpango siyo wanaostahili, hatua zimekuwa zikichukuliwa mara moja. Hata hivyo, pamoja na hayo, tunapoenda kutekeleza awamu ya tatu, mpango huu wa awamu ya tatu, tumeendelea kuhakikisha kwamba, mifumo inakwenda kuboreshwa na ushirikishwaji, ikiwa ni kipaumbele kwa wananchi husika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza!

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kwa sensa zilizopo; Watanzania kaya maskini ni karibu milioni 3.9, lakini kwenye Mpango wetu wa Bima ya Afya kwa Wote tumechukua watu wa *TASAF* wa kaya 278,000. Ni nini sasa watu maskini waliobaki ambao wanahitaji kupewa msaada wa Bima ya Afya kwa Wote?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nijibu swali la Mheshimiwa Getere kuwa katika utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, katika awamu ya kwanza, Serikali imechukua jumla ya kaya 276,000. Hivyo, tunapoenda kutekeleza awamu ya pili ya bima ya afya, ambayo juzi tu imezinduliwa kule Mtwara na Mheshimiwa Waziri wa Afya, kaya zaidi ya 600,000 zitakwenda kuingizwa kwenye Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote. Tunapoenda kutekeleza au kufikia Mpango huu wa Bima ya Afya, zaidi ya kaya 931,000 zitaingizwa kwenye Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, swali la nyongeza!

MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza;-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu huu wa kusaidia kaya masikini kwa mpango wa *TASAF*, kumekuwa na malalamiko ya kwamba, kaya zinazosajiliwa nyingi ni zile ambazo hazijakidhi vigezo, ambazo zinakuwa na uwezo, lakini pia, zile ambazo zinakuwa na vigezo vya kutokuwa na uwezo zinakuwa hazijasajiliwa! Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba, kaya zilizo maskini ndizo ambazo zinasajiliwa katika mpango huu, ili kuhakikisha fedha hizi zinawafikia walengwa? Ninashukuru.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Nuwas:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye maswali yaliyotangulia kwamba, mpango huu wa *TASAF* katika kutambua kaya za walengwa, tunatumia mfumo shirikishi. Jamii inashirikishwa kwa sababu, ndiyo wanaowajua wahusika halisi wa eneo husika kwa hiyo, tunapokwenda kutekeleza mpango huu wa awamu ya tatu, bado tutatumia utaratibu ule wa kuhakikisha jamii inashirikishwa ipasavyo kwa kupitia viongozi wao wa kijamii na wa Serikali ya Kijiji na Mitaa, ili kuwabaini walengwa, hasa ambao wataingizwa kwenye mpango na wenye sifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Regina Qwaray, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, Wizara ya Kilimo. Sasa ninamwita Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, aweze kuuliza swali lake.

Na. 40

Mapato na Matumizi ya *Export Levy*
Inayoenda Bodi ya Korosho

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA aliuliza:-

Je, Bodi ya Korosho imepokea fedha kiasi gani inayotokana na *Export Levy* tangu kurejeshwa kwake, na imetumikaje?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungahela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 hadi mwaka wa fedha 2025/2026, Bodi ya Korosho Tanzania imepokea jumla ya shilingi 363,027,429,479.70 za *export levy*. Kati ya hizo, shilingi 183,575,763,964.99 zimepokelewa katika mwaka wa fedha 2024/2025, na shilingi 179,451,665,514.80 zimepokelewa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi ya fedha za *export levy,* hadi kufikia Juni 2026 shilingi 349,310,895,502.06 zimetumika kulipa madeni ya wazabuni wa pembejeo za korosho zilizotolewa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku, kuanzia msimu wa mwaka 2022/2023 hadi msimu wa mwaka 2025/2026. Aidha, shilingi 13,373,600,759.53 zimetumika kugharamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa kupitia Bodi ya Korosho, pamoja na shilingi 342,933,218.11 zimetumika kulipa madeni ya wakulima waliokuwa wamekosa malipo ya mauzo ya korosho msimu wa mwaka 2017/2018 kutokana na kufilisiwa kwa iliyokuwa Benki ya Wanawake ya *Covenant*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Issa Mchungahela, swali la nyongeza!

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na swali moja lenye (a), (b), na (c)…

MWENYEKITI: Maswali ya nyongeza ni mawili Mheshimiwa!

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naam! Ni swali moja ndiyo! Nimeuliza swali moja lenye (a), (b) na (c). *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Issa Mchungahela, maswali ya nyongeza ni mawili, na hayana vipengele vya (a), wala (b), wala (c)! Unauliza maswali mawili ya nyongeza, ndiyo kanuni zetu ziko hivi.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Basi nitauliza maswali mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama majibu ni sahihi, kuna shilingi 240 ambayo inakatwa katika mjengeko wa kilo ya korosho. Sasa pesa hii ni ya nini? Inafanyiwa kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwenye majibu pale tumeona kwamba, kuna pesa ambazo zimelipa deni la benki; yaani benki ilikuwa inadaiwa na wananchi kwa hiyo, sasa benki wamefilisika, wanashindwa kulipa! Sasa imetumika hii pesa kulipia deni hili. Kuna uhusiano gani kati ya deni la mtu binafsi, la benki, na pesa inayokatwa, ya wananchi, kwenye kilimo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru kaka yangu, Mheshimiwa Mchungahela, kwa maswali yake mazuri ya msingi. Ninakiri kwamba, Mheshimiwa Mchungahela amekuwa akifuatilia sana suala la *export levy,* kutaka kujua uwazi na matumizi yake, hususan, kwa wakulima wa korosho:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shilingi 240 ya mjengeko wa kilo ya korosho, anafahamu matumizi yake. Moja ya matumizi ni pamoja na kwenye malipo yale, ambayo tumekuwa tunafanya kwenye mambo ya pembejeo ambazo zimekuwa zinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hizi fedha za *export levy* ambazo zimetolewa miaka ya nyuma, zilikuwa ni za kulipa madeni ya nyuma, yale ambayo yalikuwa yamejitokeza, na ndiyo maana utaona hapa tumeainisha yale madeni yaliyokuwa kati ya mwaka 2022/2023 mpaka mwaka wa fedha 2025/2026, na ndicho kilichofanyika. Kwa hiyo, na sasahivi matumizi yake, ambayo tumekuwa tunayafanya kwa wakulima, na bahati nzuri, bodi kupitia vilevile Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa tunashauriana mara kwa mara kuhusu matumizi, na tumekuwa tunafanya mabadiliko mara kwa mara; sisi tumekuwa tuko wazi katika kuhakikisha kwamba, tunamsaidia mkulima, hususan, kutokana na hii fedha ambayo inakatwa katika mjengeko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhusiano wa deni la benki ni kwamba, Benki ya *Covenant* ilipofilisika kulikuwa na wakulima

ambao katika mwaka wa fedha 2017/2018 walikosa malipo kabisa na kufilisiwa na Benki ya *Covenant* kwa sababu ya mikopo iliyokuwepo pale, na kwa sababu, tulipata maelekezo ambayo yalikuwa yanataka wale wakulima ambao waliingia hasara kutokana na zao la korosho, walipwe. Ndiyo maana bodi, kupitia Bodi ya Korosho, tukalipa haya madeni ya shilingi milioni 342, ili kuwaondoa wale wananchi na ile adha, ambayo ilikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yalikuwa ni sehemu ya maelekezo, Waheshimiwa Wabunge wanafahamu. Tuliondoa ile *risk* ambayo wakulima wale walikuwa wameipata.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Katani Katani, swali la nyongeza!

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa msimu wa 2021/2022 na 2022/2023 *export levy* ilikuwa inatolewa kwa 15%, tofauti na sasa, baada ya kubadilisha sheria ambayo 100% yote inaenda kuhudumia zao. Je, Serikali iko tayari kutafuta fedha sehemu nyingine, ili tuweze kulipa madeni haya ya 2021/2022 na 2022/2023, ili tuondoe, sasa msimu ujao, kukata makato haya ya shilingi 250, ambayo mkulima anaendelea kukatwa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampongeza kaka yangu, Mheshimiwa Katani Katani, Mbunge wa Tandahimba. Ninajua ni wadau wazuri sana wa korosho, na wamekuwa wakipigania sana maslahi ya wananchi wao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe shaka, jukumu letu ni moja tu; tumekuwa na vikao vya bodi kwa kushirikiana pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wanaotokea mikoa ambayo inazalisha korosho. Katika yale mapitio ambayo tumekuwa tunafanya kila mwaka, tutaendelea kuyazingatia mawazo, ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali muda wote tuko tayari kutafuta fedha, lakini tunapokuwa tunakosa fedha kwenye chanzo kimoja, maana yake ni tutarudi kwenu ninyi wadau, walau tujadili pamoja, mtuoneshe maeneo gani ambayo tunaweza tukapata hizo fedha, ili tuweze kumuondoa mkulima na hii adha. Kwa hiyo, Serikali muda wowote tuko tayari, kwa ajili ya kukaa pamoja na wadau na kufanya maboresho yoyote, ambayo yatakuwa na tija kwa wakulima wa korosho.

MWENYEKITI: Mheshimiwa David Silinde, Naibu Waziri, Kilimo; tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha. Sasa ninamwita Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, Mbunge wa Kigoma Mjini, aulize swali lake!

Na. 41

Ukuaji wa Uchumi Kuonekana Kwenye Kipato cha Wananchi

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha ukuaji wa uchumi unaonekana kwenye kipato cha wananchi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuimarisha ukuaji wa uchumi, zinazofungamanishwa na maendeleo ya wananchi, licha ya

kuwepo kwa misukosuko katika uchumi wa dunia kwa miaka ya hivi karibuni; kama vile janga la UVIKO 19, vita kati ya Urusi na Ukraine, kubadilika kwa sera za biashara za nchi washirika wa biashara, na vita inayoendelea Mashariki ya Kati. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi, uwekezaji katika miundombinu ya kiuchumi na kijamii (kama vile miradi ya kielelezo ya *SGR*, daraja la Kigongo Busisi, Bwawa la Umeme la *Julius Nyerere Hydro-Power Station*, utoaji wa ruzuku ya mbolea na pembejeo za kilimo, pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia jitihada hizo, ukuaji wa uchumi nchini umeendelea kuimarika na kufikia asilimia 5.9, mwaka 2025, ukilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2024, na unatarajiwa kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya Mwaka 2026 (Januari - Juni), uchumi ulikua kwa asilimia 6.3 ikilinganishwa na asilimia 5.9 kipindi kama hicho mwaka 2025. Aidha, mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja, wa wastani wa asilimia 3 – 5, ambapo kwa kipindi kilichoishia Septemba 2026, ulikuwa asilimia 4.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi unapimwa kutokana na shughuli mbalimbali zinazofanywa na wananchi, ikiwemo ujenzi, kilimo, uzalishaji viwandani, uchimbaji madini, na huduma za kijamii zinazotolewa na Serikali, ikiwemo elimu, afya na maji; kipato cha mwananchi kinaweza kuonekana kupitia ushiriki katika shughuli hizo. Aidha, maeneo mengine huwezi kuona kipato moja kwa moja kwa kuwa, Serikali hutumia sehemu ya pato hilo kutoa huduma mbalimbali, ili kujenga uchumi shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani, Serikali inaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, utoaji wa elimu msingi bila ada, mikopo ya elimu ya juu, na kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo. Hatua hizi zinasaidia kuboresha maisha ya wananchi wa matabaka yote wenye ajira na wasio na ajira *(inclusive growth)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia, inaendelea kutekeleza progamu za kuwawezesha wananchi kiuchumi, ikiwemo; utoaji

wa mikopo kwa vijana, wanawake, na watu wenye ulemavu, kupitia mikopo itolewayo na 10% ya mapato ya halmashauri, ukiongeza na ile asilimia 5, inakuwa 15, lakini tunaweka hii 10%, ambayo inaenda moja kwa moja kwa walengwa, na asilimia 5 inaenda kwenye kuboresha miundombinu na uanzishaji wa Mfuko wa Machinga, wa kuwezesha upatijanaji wa mitaji ya wafanyabiashara wadogo (machinga). Aidha, wananchi wameendelea kunufaika na utekelezaji wa kanuni za ushirikishwaji wa wazawa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini *(local content)* kwa kupata fursa za ajira.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Clayton Chipando, swali la nyongeza.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na mimi ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tumekuwa tukipokea malalamiko mengi sana ya wananchi mtaani kwetu wakizungumzia suala la *limit* kwenye miamala yao hasa miamala ya simu. Sasa hivi ukitaka kulipa, ukilipa mpaka shilingi 5,000,000 huwezi kuongeza wanakwambia kikomo chako cha siku kimefika. Ukitaka kupokea pesa kwenye simu, ukipokea shilingi 10,000,000 huwezi kupokea hela zingine wanasema kikomo chako kimefika,

Je, Serikali haioni inarudisha nyuma juhudi za kuzuia suala la kutumia *cash* kwenye malipo na kwenda kwenye *cashless* kwa kuwawekea watu *limit* kwenye namna ambavyo wanafanya malipo? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili, wananchi wa kawaida wakitaka kuongezewa *limit* ya kulipa wanalazimishwa wafungue laini nyingine ambayo inakuwa ni lipa namba, Serikali haioni inawalazimisha wananchi kuwa na laini mbilimbili mtu ambaye siyo mfanyabiashara lipa namba ya nini? Je, Serikali haioni haja ya kuongeza *limit* kwa wananchi kuweza kufanya malipo kutoka shilingi 10,000,000 kwenda mpaka shilingi 20,000,000 au shilingi 50,000,000 na kuweza kupokea mpaka shilingi 100,000,000 kwenye simu zao? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Revocatus Chipando kwa namna ambavyo anawapambania wananchi wake wa Kigoma Mjini na hakuna asiyejua hekaheka anazoendelea nazo kule na wengi tunayo mengi ya kujifunza kutoka kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, mimi ninafahamu Mheshimiwa Chipando ni mfanyabiashara, kwa hiyo analiongelea pia hili kundi la wafanyabiashara kuhusiana na misukosuko wanayopata kwenye ulipaji wa pesa kidogo kupitia mifumo ya kidigiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kupunguza matumizi ya fedha taslimu kwa kuimarisha matumizi ya mifumo ya malipo ya kidigiti ili kuongeza ufanisi, usalama, uwazi katika miamala, na ujumuishi wa wananchi kwenye huduma za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yake mawili nitayachanganya kwenye jibu moja kwa sababu yanafanana. Serikali inatambua umuhimu wa kuongeza viwango vya miamala ya fedha kwa njia ya simu ili kurahisisha malipo pia kuchochea biashara na kupunguza matumizi ya fedha taslimu hata hivyo, tofauti ya viwango vya miamala kati ya huduma za fedha kwa simu ukilinganisha hasa na mitandao ya *internet*, kwa *internet* unaweza ukalipa pesa nyingi zaidi kuliko hiyo shilingi 10,000,000 ambayo Mheshimiwa Chipando anaiongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulinda sasa usimamizi kwa sababu *internet* utaratibu wake wa kusimamia vihatarishi, utambuzi wa wateja, na usalama wa miamala ni tofauti na usimamizi wa vihatarishi kwenye mitandao ya simu, kwa mujibu wa Kanuni ya Fedha za Kieletroniki za mwaka 2015, Benki Kuu ina mamlaka ya kuweka na kuboresha viwango hivyo kwa kuzingatia aina ya mteja na aina za udhibiti wa vihatarishi, ikiwemo na utakatishaji kwa mfano, kuna *issue* za utakatishaji wa fedha,

ubadhirifu na udanganyifu wa fedha, kwenye mitandao ya simu ukaweza kulipa shilingi 100,000,000 na namna ambavyo mitandao ya simu uratibu wake na udhibiti wake bado unafanyiwa kazi inaweza ikaleta hasara kwa wafanyabiashara ambao wanafanya malipo kwa simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Benki Kuu inaendelea kuboresha mifumo ya malipo na inafanya tathmini ya uwezekano wa kuongeza viwango hivyo vya miamala kwa njia ya simu kwa kuzingatia mahitaji ya biashara kama ambavyo Mheshimiwa Chipando ameelezea lakini pia kuzingatia maendeleo ya kidigiti. Bado tunaendelea kujifunza mifumo ya kidigiti ya kulinda usalama wa fedha za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha miamala ya thamani kubwa kufanyika kwa urahisi na usalama basi ni mpaka hapo ambapo mifumo yote itakuwa imewekwa vizuri. Mheshimiwa Chipando uwe na amani Serikali inajali wafanyabiashara, Serikali inajali wananchi lakini lazima wananchi walindwe na vihatarishi ambavyo vinaweza vikatokana na miamala ya kupitia simu. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Mshamu Munde, Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea ninaomba niwatambulishe wageni waliopo Jukwaa la Spika, wageni wanne kutoka Baraza la Wawakilishi ambao ni Ndugu Hassan Ali Haji, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar; Ndugu Othman Ali Haji, Mkurugenzi Idara ya Shughuli za Baraza; Ndugu Maryam Hussein Rajab, Mkuu wa Kitengo cha Habari, Mawasiliano na Uhusiano; na Ndugu Masoud Ali Hamad, Afisa Uhusiano kutoka Baraza la Wawakilishi. Karibuni sana wageni wetu kutoka Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa ninamwita Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, aweze kuuliza swali lake.

Na. 42

Kuanzisha Mamlaka Inayosimamia *Unclaimed Financial Assets* - Tanzania

MHE. FESTO R. SANGA aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Mamlaka ya kusimamia *Unclaimed Financial Assets* hapa nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mali ambazo hazijadaiwa ni mali au fedha zinazoshikiliwa na benki, taasisi za fedha, kampuni za bima, kampuni za uwekezaji, mifuko ya hifadhi ya jamii au taasisi nyingine za fedha, ambazo hazijadaiwa na mmiliki halali kwa kipindi maalumu kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mali ambazo hazijadaiwa zinaweza kutokea kutokana na kifo, kusahau, utunzaji mbaya wa kumbukumbu, kuhama, kutokujua kwa mmiliki au mtu anayestahili kuipokea mali hiyo, uzembe wa mmiliki au mtu anayestahili kuipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaweza ikawa pia kupotea kwa mawasiliano, kuunganishwa kwa kampuni au taasisi *(mergers),* na ukosefu wa taarifa au uelewa kuhusu uwepo wa mali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mali ambazo hazijadaiwa zinasimamiwa na sheria mbalimbali za sekta ya fedha pamoja na wasimamizi wa sekta ya fedha ambayo ni Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania na taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha mfumo wa usimamizi wa mali ambazo hazijadaiwa imeandaa andiko dhana la mapendekezo ya kuboresha mfumo wa kisheria wa usimamizi wa mali hizo. Kwa sasa, Wizara ya Fedha ipo katika hatua ya kufanya uchambuzi wa kina na kupata maoni ya wadau mbalimbali kutoka Serikalini na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nitakuwa na swali moja tu lakini kabla sijauliza hilo swali Mheshimiwa Naibu Waziri na afahamu kwamba hii imekuwa ni hoja yangu na nimekuwa nikizungumza takribani mwaka wa sita sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba nchi yetu imekuwa na changamoto ya kutokuwa na *clarity* kwenye hilo suala la upatikanaji wa hizo fedha. Kwenye ripoti ya *CAG* ya mwaka 2022/2023 imezungumza kati ya benki 21 ni benki tano tu ndiyo zimeripoti kwamba kuna fedha ambazo hazijafuatiliwa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba, kuna mianya inayoonesha kwamba ufuatiliaji wa hizi fedha ambazo ni *unclaimed* haujafanyika kiuhalisia tofuati na nchi za Kenya Uganda, Rwanda, *South Africa*, na Morocco ambako nimefanya *research* kujua hiki kinachoendelea. Mheshimiwa Waziri ninawapongeza kwamba mmeanza mchakato lakini mchakato huu ni wa kisheria, tunatamani kuwa na mamlaka kwa sababu dunia ya sasa ni ya *cashless economy*. Watu wengi wanaweka

fedha kwenye simu, wanaweka fedha kwenye maeneo mbalimbali ambapo familia hazijui kwamba huyo mtu ana hela kwenye eneo hilo au hana eneo hilo. Kwa hiyo, ukusanyaji wa fedha umekuwa ni mgumu kutokana kwamba sheria zimekuwa hazifuatiliwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni moja, mbali na fedha lakini kumekuwepo na viwanja, nyumba lakini pia bodaboda *for instance* nitatoa mfano mmoja tu. Kuna kijana wa bodaboda unakuta amekuja mjini kutafuta maisha, amenunua pikipiki yake amepata ajali bahati mbaya amefariki pikipiki yake imeenda polisi kwa muda mrefu haifuatiliwi na ndugu hawajui kwamba kuna hicho kitu.

Je, Serikali katika huu mchakato mnaoendelea nao mna-*include* pamoja na hili ili iweze kutengeneza mazingira ambayo hizi fedha ambazo ni matrilioni, watanzania wanakuwa wanazitambua na baadaye ziweze kurudi ama kwa familia kupitia miradi au Serikali iweze kutafuta namna nyingine ambayo inaweza kuzitumia? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Festo Sanga. Mimi ninajua kwamba Mheshimiwa Festo Sanga amekuwa akifuatilia kuhusiana na *unclaimed assets* kwa miaka mingi. Hata Bunge la Nne aliuliza swali na Wizara ya Fedha inafanya jitihada za kufuatilia masuala ambayo anayafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa mali zisizohamishika zinaweza kuwa za kifedha katika akaunti zisizotumika lakini pia zinaweza zikawa mali ambazo amezielezea kama vile viwanja, nyumba, magari na pikipiki; ametumia bodaboda, kama mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mali zisizo za kifedha zinasimamiwa kupitia sheria na mamlaka mbalimbali kulingana na aina ya mali husika. Kwa mfano, Sheria ya Kushughulikia Ukiukwaji

wa Masharti ya Umiliki wa Ardhi ikiwemo ardhi isiyoendelezwa kwa mujibu wa masharti hayo, ardhi ina sheria ya kusimamia mali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Sheria ya Usalama Barabarani ya Sura Na. 168 inaweka utaratibu wa kushughulikia magari yaliyotelekezwa. Kwa hiyo, ukiangalia hapa, mpango wa Serikali kwa sasa wa kuandaa mfumo wa kitaifa wa kusimamia mali zisizodaiwa unalenga hasahasa katika masuala ya kifedha, lakini inaenda kuboresha ule utaratibu ambao unahusisha zile bidhaa ambazo siyo za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mali hizo sasa zisizo za kifedha, Serikali itaendelea kutumia mfumo wa kisheria uliopo huku ikitathmini maeneo yanayohitaji maboresho ili kuimarisha utambuzi, utunzaji na urejeshaji wa mali kwa mhusika ambaye anatakiwa amilikishwe mali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy Kombani, swali la nyongeza.

MHE. LUCY D. S. KOMBANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Hili suala la mali zisizodaiwa *(unclaimed assets)* bado ni geni kwa watanzania wengi sana kitu ambacho kinadhoofisha mchakato mzima wa kuzidai mali hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua Wizara inatumia utaratibu gani katika kuhakikisha wananchi wanapata elimu kuhusu mali hizi na namna ya kuzidai?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kombani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, tunaandaa utaratibu wa kuratibu mali zisizodaiwa. Katika kufanya hivyo, kwa kuwa tunashirikisha sekta za Serikali na sekta binafsi, kwenye andiko, dhana ambayo inaandaliwa na uchambuzi

ukifanyika utahusisha pia kuelimisha wananchi kuhusiana na namna ya ku-*claim* bidhaa au mali isiyodaiwa kwa maana ya fedha na zile bidhaa nyingine kwa mujibu wa Mheshimiwa Festo Sanga, kama nilivyoelezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Arif Premji, swali la nyongeza.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia fursa niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninamsikiliza Mheshimiwa Waziri kuanzia alivyopanda kwenye *podium* mpaka mwisho na alizungumzia kuhusiana na ukuaji wa uchumi kwamba Taifa letu linakua kiuchumi kwenye suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na ukuaji wa kiuchumi lakini hapohapo ripoti ya Septemba ya *NCPI* inaonesha gharama za maisha kupanda, ilikuwa ni alama inaonesha 119.86 kufikia 125.07 yaani gharama ya maisha ya Mtanzania inapanda pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mfuko wa mwananchi unaguswa kwa gharama za bidhaa, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ina mpango upi madhubuti wa kikodi *(Fiscal Policy)* ili iweze kudhibiti bei za bidhaa zinavyopanda na faida au fedha ile iingie kwenye mfuko wa mwananchi wa kawaida? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Premji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimeongelea kuhusu ukuaji wa uchumi na Mheshimiwa Premji ni mfuatiliaji sana wa masuala ua uchumi na yeye mwenyewe *of course* ni mfanyabiashara. Ni kweli kwamba ukiangalia *CPI* kwa maana ya mabadiliko ya

gharama za maisha kuna *element* ya ukuaji wa gharama za maisha kwa mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali kupitia Wizara ya Fedha inafanya utaratibu kwa kutunga sera na sheria wezeshi ili kudhibiti mfumuko wa bei ambao unaenda kumdhuru mwananchi wa kawaida. Kwa hiyo, zipo *policies* kama alivyoongelea *fiscal policies* ambazo zinachunga ukuaji wa mfumuko wa bei ambao mpaka saa hivi kama nilivyotangulia kusema tuko bado kwenye tarakimu moja kati ya asilimia tatu mpaka tano ambayo kwa kweli kwa hapa Afrika Mashariki sisi ni vinara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema Serikali inaendelea kuweka sera, sheria na kanuni za utekelezaji wa masuala ya kiuchumi ili kudhibiti hali hiyo ya mfumuko wa maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea swali letu la mwisho kwa siku ya leo litaulizwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 43

Udhibiti wa Michezo ya Kubahatisha

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO aliuliza:-

Je, Bodi ya Bahati Nasibu ina mpango gani wa kudhibiti michezo ya kubahatisha (madugudugu ya Wachina) inayodaiwa kuharibu maadili nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maluum, kutoka Mkoa wa Tanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya michezo ya kubahatisha hapa nchini inasimamiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania *(GBT)*. Sekta hii imekuwa ikikua kwa kasi na imekuwa na mchango mkubwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali hali kadhalika maendeleo ya jamii. Hata hivyo, zimejitokeza changamoto kadhaa, hususan katika uendeshaji na usimamizi wa biashara ya *slot machines* (maarufu kama madubwi) kwa wale ambao wanacheza. Kumeongezeka shughuli za michezo hii katika maeneo yasiyokuwa rasmi hasa maneno ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na hali hii, bodi imechukua hatua zifuatazo:

(i) Bodi imesitisha utoaji wa leseni mpya kwa waendeshaji wa kigeni wanaendesha michezo ya *slot machine* (madubwi), ili kutoa nafasi ya kufanya tathmini ya kina ya athari zake kijamii na kiuchumi pamoja na kuimarisha mifumo ya udhibiti;

(ii) Bodi inakusudia kuingia katika makubaliano ya ushirikiano, (*Memorandum of Understanding* – MoU), na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa michezo hiyo, hususan katika maeneo ya vijijini na katika ngazi za Serikali za Mitaa, ambapo udhibiti ulikuwa na changamoto kutokana na ueneaji usio rasmi;

(iii) Bodi imeanza mchakato wa kuweka mfumo maalum wa kiteknolojia wa kuratibu na kudhibiti mashine za michezo ya kubahatisha *(slot machines monitoring system)*, ambao utawezesha ufuatiliaji wa moja kwa moja ya uendeshaji wa mashine hizo pamoja na kuhakikisha kuwa zinazingatia masharti ya kisheria na viwango vilivyowekwa;

(iv) Serikali kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, Mamlaka ya Mapato Tanzania, pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imekuwa ikiendesha operesheni maalum za kuwabaini na kuwachukulia hatua waendeshaji haramu wa michezo hiyo, ambao kwa kiasi kikubwa wanachangia tatizo hilo. Hadi sasa, jumla ya mashine 1,702 zimekamatwa na kuharibiwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita;

(v) Bodi inaongeza juhudi za utoaji elimu kwa umma, hususan kwa vijana, kuhusu madhara ya matumizi holela ya michezo ya kubahatisha, ikiwa ni pamoja na athari zinazotokana na kushiriki kwa michezo hiyo bila kuzingatia *responsible gaming*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa ujumla Serikali kupitia bodi itaendelea kuimarisha usimamizi wa sekta hii ili kuhakikisha uendeshaji wake unazingatia sheria, kanuni, na kulinda maadili ya jamii pamoja na maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza, ninaishukuru Serikali kwa kuona ipo changamoto na kuanza kuifanyia kazi. Ninakushukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yako, uniruhusu niulize maswali mawili.

Swali la kwanza, kwa kuwa tayari wameonesha kusudio la kuingia kwenye makubaliano na Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuendesha kwa pamoja michezo hii, nilitaka kujua ni lini sasa watasaini hayo makubaliano ili kuwapa wenzetu wa Halmashauri nafasi ya kusimamia michezo hii? Kwa sababu inachezwa kule chini kwenye mitaa, kwenye nyumba binafsi wanapoishi watoto wadogo na wanapata madhara makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; kwa kuwa tunafahamu michezo hii*, Gaming Board* inalenga kukusanya pia mapato ya Serikali, lakini mmomonyoko wa maadili unaosababishwa na michezo hii ni mkubwa.

Je, Serikali katika tathmini ambayo wanaifanya, ni pamoja na kuona kama kuna umuhimu mkubwa wa kukusanya mapato kuliko ule wa kuzuia huo mmomonyoko wa maadili ambao unaendelea katika nchi yetu? Ninakushukuru.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. *ENG*. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Husna, ambaye ninaona anajali sana na kama ambavyo Taifa linajali sana kesho ya vijana, hasa wanaojihusisha na shughuli za biashara ya hiyo ya bahati nasibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini kwamba makubaliano hayo yatasainiwa? Bado rasimu inaendelea kuchakatwa lakini pia tunataka kupata maoni ya wahusika (Mamlaka za Serikali za Mitaa), na wadau wengine ambao ni sekta binafsi, ili tuone makubaliano hayo yanaweza yakawa yame-*contain elements* zote ambazo zinahitaji kuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *elements* hizo kwa mfano, sasa hivi kwenye michezo hiyo ya kubahatisha ambayo yale madubwi yanayowekwa kwenye vijiji na maeneo ya biashara, Halmashauri haipati mapato kutoka kwenye hizo dubwi. Pia, Halmashauri haitoi leseni za biashara hizo, biashara inatolewa na *Gaming Board.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunataka kuangalia wadau watapendekeza nini ili kwanza kuwa na *sharing* ya mapato, pia kuangalia ku-*mitigate* zile changamoto ambazo zilikuwepo kwa ufasaha zaidi. Kwa hiyo, ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba makubaliano yatasainiwa hivi punde, lakini baada ya kuwa wadau wote wameshirikishwa na

kuangalia *elements* zote ambazo zinaleta changamoto, pia katika *sharing* ya mapato ya hizo dubwi iweze kuwa stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye suala la pengine Serikali inaona bahati nasibu ni faida zaidi kuliko mmomonyoko wa maadili. Hadi sasa hakuna utafiti wala ushahidi unaoonesha kuwa michezo hii ya kubahatisha inachangia mmomonyoko wa maadili. Sasa hili niliweke wazi kidogo, tafiti zilizofanyika zinaonesha kuwa, madhara makubwa yanayotokana na biashara ya dubwi ni uraibu. Uraibu kwa maana ya *addictions*. Vijana wanakuwa sasa *addicted* kucheza hiyo michezo. Sheria ya Kubahatisha Sura 41 inaipa *GBT* jukumu la kulinda jamii, wakiwemo watoto, dhidi ya madhara hayo ya uraibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti hilo, ziko taratibu ambazo *GBT* inazifuatilia. Kwa mfano, dubwi haichezwi na watoto chini ya miaka 18. Niendelee?

MWENYEKITI: Ndiyo, Mheshimiwa. Malizia kutoa ufafanuzi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukizingatia hayo niliyoyasema, kwamba mmomonyoko wa maadili kwa njia ya biashara ya dubwi haupo; uraibu unaendelea kuwa *mitigated* na taratibu ambazo zinadhibitiwa na *Gaming Board.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Mushamu Ali Munde, ninakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Ninaomba kukumbusha tu mambo machache yafuatayo:-

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Ninaomba kukumbusha mambo machache yafuatayo:

Waheshimiwa Wabunge, Mbunge anapopata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, swali lake la nyongeza ni muhimu likaendana na swali la msingi. Mbunge ambaye ana swali la msingi, maswali yake ya nyongeza yanapaswa kuendana na swali lake la msingi. Hiyo ni muhimu tukakumbushana ili pia kuwapa nafasi Mawaziri watoe majibu sahihi na kwa ufasaha kutokana na maswali ambayo Wabunge tumeyauliza.

Baada ya kusema hayo, ninaomba niwatambulishe wageni walioko Bungeni, ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Yupo mgeni mmoja wa Mheshimiwa Simon Songe, ambaye ni Ndugu Mustafa Hassan, rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Suma Fyandomo, ambao ni wapiga kura kutoka Jijini Mbeya. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Amour Seif Abdallah, ambaye ni Ndugu Bahati Hamis Shaban, mfanyabiashara wa vifaa vya magari kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wageni nane wa Mheshimiwa Amour Seif Abdallah, ambao ni wanachama wa Umoja wa Mafundi Magari Tanzania kutoka Wilaya ya Kinondoni, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watatu wa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, ambao ni Masheikh wa Kata kutoka Jimbo la Chamazi, Mkoani Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 11 wa Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, ambao ni viongozi wa Chama cha Wenye Ualbino Tanzania pamoja na viongozi wa Jumuiya ya Wasioona kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 12 wa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Jimbo la Urambo, Mkoani Tabora. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; yupo Ndugu Baraka Emmanuel pamoja na Ndugu Najma Zuberi kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Osward Mwakabugila, ambaye ni Afisa Elimu – Taaluma kutoka Halmashauri ya Mji Tunduma, Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 46 na walimu sita wa Shule ya Sekondari Magole kutoka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wapo pia vijana 45 wa Shirika la *Youth Development Organization* kutoka Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wageni wetu, karibuni sana hapa Bungeni Dodoma.

Katibu!

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028
na
Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tunaendelea na majadiliano. Sasa ninamwita Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi

Muhongo; atafuatiwa na Mheshimiwa Sara Msafiri Ally na Mheshimiwa Adonis Alfred ajiandae.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunikaribisha. Waheshimiwa Wabunge, nitaomba kidogo huyu jirani yangu amenipatia muda wake ametoka, kwa sababu mchango wangu una takwimu, kwa hiyo, mchango wenye takwimu unahitaji muda. Kwa hiyo, Waheshimiwa vumilieni maana siyo maneno matupu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tumsikilize Profesa.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sasa, Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba hapa tunatoa ushauri na kweli tutoe ushauri. Ndiyo tunavyotegemewa hivyo, wa mpango na bajeti inayokuja ya mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nianze kutoa angalizo, ukweli Serikali zote na Serikali yetu lazima zinajitahidi kufanya kazi, lakini wanahitaji mawazo ya kuboresha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa anajitahidi na timu yake lakini lazima tuendelee kumshauri na kumuongezea. Leo siyo siku ya kuongelea mambo ya jimboni, lakini tu kwenye mambo ya mipango sisi Musoma Vijijini tuna matatizo yetu sugu; la kwanza ni barabara, la pili ni maji. Sasa uzuri ndugu zangu wa *TANROADS* wamenihakikishia kwamba hata mambo ya barabara hapa nisiongelee, tutamalizana nao huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya mipango yanahitaji fedha. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tunachopaswa kuishauri Serikali na kusaidia Tume ya Mipango ni namna ya kupata fedha nyingi za miradi. Wabunge wote hapa majimboni kwetu sasa hivi Tanzania nzima, fedha zinahitajika sana kwenye miradi ya barabara na miradi ya maji. Pengine kote tunaenda vizuri, hayo wawili hayo; barabara na maji. Tupo kwenye *Vision 2050,* yaani malengo yetu yote yanahitaji fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka niwapatie hapa takwimu za kuonesha tunaendaje, kwa nini tunaenda polepole, na tufanyeje. Nimeangalia uchumi wetu wa watanzania tangu mwaka 1960 mpaka leo hii. Sasa hapo ndiyo ninaomba tusikilizane vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1960, uchumi mzuri unauangalia kwenye miongo miwili miwili. Hakuna uchumi duniani unaenda kwa miaka mitano au miaka 10, haijawahi kutokea hiyo. Ni miaka 20 na kuendelea mbele. Mwaka 1960, Tanganyika tulikuwa watu milioni 10.1. Mwaka 1980, Tanzania tulikuwa watu milioni 19.2. Ongezeko la wananchi, ongezeko la watu Tanganyika mwaka 1960 ilikua kwa 2.8%. 1980 ongezeko lilikuwa 3.1%. Takwimu hizi ni muhimu sana kujenga hoja huko tunapoenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi mwaka 1960, ndiyo *World Bank* ilikuwa inaanza mambo ya kuangalia ukuaji wa uchumi duniani. Mwaka 1961 uchumi wetu umekua kwa 1.14%. Mwaka 1962 hatujawahi kufika hapo mpaka leo hii, ndiyo uchumi ulikuwa kwa 9.1%; hatujawahi kupata uchumi kama huo. Mwaka 1980, ukuaji wa uchumi ulikuwa 3.3%. Pato la mtu mmoja mmoja mwaka 1960, *GDP per capita,* ilikuwa dola 275. Mwaka 1980 ilikuwa dola 611.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi takwimu siyo za mzaha. Mwaka 1960 – 1980, kwa miaka 20 watu tumeongezeka mara 1.9, karibu mara mbili. Sasa uchumi mzuri wa nchi ni lazima ongezeko la watu liendane na ongezeko la uchumi. Kwa hiyo, mwaka 1960 na mwaka 1980, ukiangalia hizo *GDP per capita,* ongezeko la miaka 20 uchumi wetu umeongezeka mara 2.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda ninaruka kwenda mwaka 2000 na mwaka 2020. Mwaka 2000 tulikuwa Watanzania milioni 33.5, mwaka 2020 tulikuwa milioni 60. Ongezeko la watu nchini mwaka 2000 ilikuwa asilimia tatu. Ongezeko la watu mwaka 2020 ilikuwa asilimia 2.8. Ongezeko kiuchumi *(GDP growth rate)* ilikuwa asilimia 4.52. Mwaka 2020 ndiyo ilikuwa ya chini, ilikuwa *2.5,* na hii ni kutokana na ile *COVID-19*, ilikuwa dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, angalia *GDP per capita* mwaka 2000 ilikuwa ni dola 402. *GDP per capita* mwaka 2020 ilikuwa dola 1,117. Kwa hiyo, ongezeko la watu kati ya mwaka 2000 na mwaka 2020 ilikuwa mara 1.8. Ongezeko la pato la mtu mmoja mmoja kwa hiyo miaka 20 ilikuwa mara 2.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja sasa kwenye hoja yangu, nimechukua miaka minne ya mwisho; mwaka 2022 na mwaka huu 2026. Mwaka mwaka 2022 tulikuwa Watanzania milioni 61.7. Mwaka huu, sasa hivi tuko Watanzania milioni 73.4. Ongezeko la watu mwaka 2022 lilikuwa 3.2, mwaka huu ni 2.9. Ukuaji wa uchumi mwaka 2022 ilikuwa *4.7 percent* na mwaka huu ni *6.0 percent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *GDP per capita* mwaka 2022 ilikuwa *1,192 dollars per person per annum*, na mwaka huu *GDP* yetu ni *1,325 US Dollars per person per annum*. Kwa hiyo, kwa miaka minne hii ongezeko la *GDP* ni mara 1.1 na ongezeko la watu ni mara 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndipo swali la hoja yangu linapokuja sasa. Tunaenda 2050; malengo yetu ya 2050*;* Mwaka huu tuko watu milioni 73.4; *2050* tutakuwa watu milioni 140. *GDP per capita* yetu sasa hivi ni *1,325 US Dollars per person per annum*. Tume ya Mipango inasema tukifika mwaka 2050 *GDP per capita* yetu inapaswa kuwa dola 7,000. Hilo ni ongezeko la mara tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali Waheshimiwa Wabunge, hata wewe uliyeko hapa, yaani mjadala tunaoufanya ni kwamba, ikifika mwaka 2050 wewe mwenyewe pato lako litakuwa ni zaidi ya mara tano. Je, ni kweli? Je, tutaweza? Ndilo swali la msingi hilo. Tunaenda kuongezeka mara tano. Sasa, jibu jepesi jepesi ni kwamba haiwezekani. Yaani kama hivyo wanavyopiga kelele kwamba Wabunge mshahara wenu ni kiasi fulani, watakaokuwepo mwaka 2050 mshahara huo uzidishe mara tano. Ndiyo maana yake hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa ndiyo ninakuja kwenye hoja. Hili linawezekana, na ndio ushauri. Mwenye saa

anza upya tena, anza upya; anza upya. Ninakuja kwenye mambo ya msingi zaidi, ushauri ambao Mheshimiwa Profesa Kitila anautaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linawezekana, tusikatishane tamaa; hata kama Taifa tusikate tamaa na profesa usikatishwe tamaa. Jibu linatoka China. China ndio walifanya miujiza duniani haijawahi kutokea. Tangu mwaka 1978 – 2005, kwa miaka 27 uchumi wa China ulikua kwa wastani wa asilimia 10 na zaidi ya asilimia 10. Miaka ambayo uchumi ulikua, mwaka 1988 uchumi wa China ulikua kwa asilimia 15.2, *growth per annum 15.2 percent*. Mwaka 1992 uchumi wa China ulikua kwa asilimia 14.3 na mwaka 2007 ulikua kwa asilimia 14.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge sisi kama Watanzania tusikate tamaa, tusikatishane tamaa, tuweke mikakati ya uchumi. Ndiyo maana unanisikia mimi ninaongea uchumi ukue kwa zaidi ya asilimia 10. Mapendekezo haya tunayoyaongeza ya tozo, tozo haijawahi kukuza uchumi duniani kote. Tuongee mambo kweli ya kitaalamu. Hakuna mahali ambapo sisi tunaofanya utafiti kila siku tunakuta sehemu sijui tozo iliwekwa ikakuza uchumi. Hapana! Uchumi unakuzwa na *production*, *commodities* unazoziuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Tanzania cha kwanza, Tume ya Mipango ndiyo itusaidie sasa. Nilipendekeza na bado iko hivyo hivyo. Kilimo ndicho ambacho kimeajiri wengi na kilimo ndicho kina viwanda. Mheshimiwa profesa alifanya vizuri, nimsikiliza, alisema tuwekeze kwenye umwagiliaji. Sasa, kilimo kikuze uchumi kama tunataka kwenda huko. *(Makofi)*

Tulieni, huwa ninaomba makofi baadaye, kwa sababu kuna takwimu watu hawatasikiliza takwimu. Utulivu! Karibu niwaambie kama mkutano wa hadhara niseme oyeeh, lakini siyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia sasa ninamalizia mapendekezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo asilimia 10; sasa, Tume ya Mipango inapaswa kutueleza ni namna gani kwenye sekta ya kilimo ichangie asilimia 10, wakati soko, kwa mfano soko upande wa kilimo, mchele *(rice)* ile *market size* ya mwaka huu, *global market size value* ya *rice* (mchele) ni dola bilioni 318.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, Tume ya Mipango inapaswa kuja na mipango kwamba, sisi tutapataje fedha nyingi kwenye hizo dola bilioni 318? Tufanyeje? Ngano soko lake kwa mwaka huu duniani ni takribani bilioni 200. Ndiyo Tunataka majibu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, ninamalizia bado kidogo tu. Cha pili gesi asilia ...

MWENYEKITI: Ninakuongezea dakika mbili za kumalizia.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante, ahsante! Inabidi niende haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, desi asilia na viwanda vyake, kila ninachosema na viwanda vyake, kilimo na viwanda vyake. Gesi asilia ichangie *25 percent of the GDP*. Sasa, tuangalie soko la gesi asilia *(natural gas)*, *global natural gas market size* sasa hivi duniani *natural gas* ni bilioni 920. Je, sisi tutaingiaje huko kuzipata hizo? Halafu *LNG* tunayoiongelea sasa hivi ni bilioni 256 na *thirty, thirty-three* itafika takribani bilioni 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uchumi wa gesi tuufanyie kazi. Tusifikirie mambo ya tozo, twende kwenye uchumi wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tatu ni madini na viwanda vyake uchangie asilimia 20. Haya, mambo ya madini duniani biashara hiyo mwaka huu, makaa ya mawe yalikuwa na thamani ya dola trilioni 1.1, *coal*. Chuma kama Liganga ikianza, bilioni 313, shaba *(copper)* bilioni 270, dhahabu ambayo tumo lakini hatujafanya sana bilioni 264.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna kingine kikubwa sana ambacho hatatufanyia kazi, simu tulizonazo na nini, zote hizi

zinatumia *semiconductor chips*. Ile biashara ya *semiconductor chips* duniani sasa hivi ni dola trilioni 1.1. Yanahitajika madini *rare earth;* hatujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni utalii na viwanda vyake vichangie asilimia 15. Sasa, mambo ya *travel* na *tourism industry* mwaka huu duniani ni trilioni 11.6. Wanaoongoza duniani ni Marekani trilioni 2.6, halafu wanakuja China, wanakuja Ujerumani. Kwa hiyo, utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, bado moja tu ninamalizia. Tano, uvuvi, ufugaji na viwanda vyake vichangie *five percent*. Mwaka huu biashara ya samaki na *seafood* ni bilioni 351. Mambo ya nyama ni bilioni 175. Tutaingiaje huko tusifikirie tozo? Twende huko tuuze nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ninakaribia ya saba. Sita ni *labour export na remittances*. Hii ni muhimu sana, *diaspora*. *Diaspora* hapa tunahitaji wa ngazi zote. Tuchukue wale wa mishahara midogo midogo wakienda nje na wale wenye mishahara mikubwa. Sasa, Afrika hao *diaspora* watuletee *three percent*. Afrika anayeongoza wa kwanza ni *Egypt*, wa pili *Nigeria*, wa tatu *Morocco*, wa nne ni *Kenya* ambaye anapata takribani bilioni tano kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni mambo ya michezo na mengineyo yatuchangie asilimia mbili. Sasa, kwa ajili ya muda, nikimaliza hapa nitawawekea kwenye *group* lile la chama, kuona mageuzi ya *China* na *India* tangu mwaka 1961 mpaka leo hii. Tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Mheshimiwa profesa mara nyingi amesema tukitaka kufanikiwa tufanye kazi isiwe *business as usual*. Suala ambalo hatujajadili humu, je, ufanyaji wetu wa kazi sasa hivi kwa mtindo huu unaweza ukatufikisha kwenye dola 7,000 kila mtu mwaka 2050? Hiyo kuna siku nitawapatia duniani watu wengine wanafanyaje kazi, wanatengenezaje fedha. Hilo ni somo la siku nyingine. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana profesa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mheshimiwa Adonis Alfred ajiandae.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachukua nafasi hii, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Prof. Muhongo kwa kutupa takwimu nzuri. Mimi nichukue nafasi hii kwa ajili ya kuchangia mpango wa maendeleo na mwongozo wa dira yetu. Ninampongeza Mheshimiwa Profesa Kitila kwa kufanya kazi nzuri katika uchambuzi na ufafanuzi kwenye maeneo mbalimbali ya dira maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianzie katika namna ya upimaji wa utekelezaji wa mambo ambayo tayari tulishakubaliana Bunge na Serikali katika utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka, Bunge la Bajeti lililopita Serikali ilishaelekeza mamlaka za Serikali ziandae angalau andiko moja kwa ajili ya miradi ya *PPP*. Serikali ilishaelekeza na Bunge tukaridhia, kwamba Halmashauri zote ziandae walau miradi mitatu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii kupitia *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu ni kweli kwamba dira yetu inaonyesha kabisa asilimia 70 ya utekelezaji wa gharama za mpango itatoka sekta binafsi. Wote kwa pamoja tulikubaliana, kwamba namna pekee ya kutekeleza mradi huu na kufikia *one trilioni dollar* kama tulivyokubaliana, ni kupitia *PPP*. Nimekuwa nikifuatilia taarifa mbalimbali za Serikali, sijaona njia nyingine yoyote mbadala ambayo inapendekezwa na Serikali katika utekelezaji wa mpango huu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu kwa Profesa ni kwamba, kama yale machache tuliyokubaliana, mamlaka za Serikali ziandae walau mradi mmoja, Halmashauri ziandae walau miradi mitatu kupitia *PPP*. Hakuna utekelezaji hadi sasa hivi. Sasa tutaendaje? Kwa sababu, mpango huu wa maendeleo unaonyesha kabisa utekelezaji wake hauwezi ukategemea

mikopo na bajeti ya ndani ya Serikali. Lazima tutafute njia nyingine mbada ya kutafuta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri atatueleza yale tuliyokubaliana mwanzo yametekelezwa kwa kiwango gani. Mimi kwa wafuatiliaji wangu hakuna hata Halmashauri iliyoleta andiko la kutenga fedha kwa ajili ya miradi hiyo, wala mamlaka za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwamba, kwa kweli mpango huu wa maendeleo unahitaji mabadiliko makubwa. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, amekuwa *champion* wa utekelezaji wa mipango hii. Kukamilika kwa miradi mikubwa ya kimkakati, reli ya *SGR*, Bwawa la Mwalimu Nyerere, kuboresha bandari zetu na zikaongeza uzalishaji mpaka sasa imekuwa changamoto kwenye barabara huko; ni namna ambavyo Mheshimiwa Rais amekuwa *champion* wa kuhakikisha kwamba anaibadilisha nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kubwa ni kwenye taasisi zetu za Serikali. Pale ambapo Mheshimiwa Rais amefanya kwa kiwango kikubwa, miradi ya trilioni imekamilika, lakini huoni taasisi za Serikali zikijibadilisha katika utekelezaji. Mamlaka za Serikali zimekuwa zikitenga fedha nyingi kwa ajili ya kuandika maandiko ya miradi, lakini kwenye miradi inayotegemea fedha za serikali; mikopo ya Serikali au kupitia kodi za Serikali. Sasa, kama fedha za kuandika miradi hiyo ya mikopo na kodi zinapatikana, kwa nini fedha za kuandika miradi kwa ajili ya kufanyika kupitia *PPP* haitekelezeki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kama tunakubaliana kuwa asilimia 70 ni sekta binafsi, na kama tunaona *PPP* bado kuna shida, tuletewe mbadala wa kutafuta fedha hizo kwa njia ya mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali, imejenga miradi mikubwa ya maendeleo ya huduma za kijamii kwa wananchi. Serikali imejenga vituo vya afya na zahanati za kisasa, shule za msingi na za sekondari za kisasa, ofisi za Serikali na taasisi

mbalimbali za umma za kisasa huko kwenye Halmashauri zetu. Hata hivyo, bado tunategemea Serikali ije ijenge nyumba ya mtumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri kwa kiwango cha chini ina idadi ya watumishi 2,000; jumlisha sasa Halmashauri zote hizo. Ni lini Serikali hii itakuja kusimama hapa ikatwambia itamaliza changamoto za nyumba za watumishi? Miradi yote hiyo ya vituo vya afya, zahanati, shule na miradi mingine kumetengwa maeneo ya kujenga nyumba za watumishi. Kwa nini miradi hii isifanyike kupitia *Public Private Partnership*? Vinginevyo tutakuwa tunaimba tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mikubwa kama ya Bwawa la Mwalimu Nyerere imekamilika, lakini bwawa lile siyo kwa ajili ya nishati tu. Tunataka kuona *irrigation*, *navigation*, utalii na mambo mengine yanaenda pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu huko duniani ukienda kwenye *Tennessee Valley* kule, ile ni *authority*; kuna mamlaka inasimamia. Anayetaka umeme aende pale akachukue umeme, akanunue. Anayetaka kufanya *irrigation* na *navigation* waende pale wakafanye. Miradi hii imekamilika lakini hatuioni ikijitanua sasa kuja kuwa vivutio vya fursa za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana profesa ambaye ni Waziri wetu, mimi ninamwamini, na amekuwa akifafanua vizuri. Shida yangu ni kwenye kutekeleza kwenye mamlaka zetu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana hapa *TANROADS* iwe mamlaka kamili. Kama mamlaka ya bandari imefanya vizuri, mimi ninaamini na *TANROADS* itafanya vizuri. Tukisema *TANROADS* ibaki na muundo huu huu na majukumu haya haya, na bado ikasimamie masuala ya *PPP* haitaweza. Kila jambo ni lazima kuwe na *bureaucracy*, madokezo, nani aridhie; hatuwezi kufika. Mimi ninaamini mafanikio makubwa ya mamlaka ya bandari ni kwa sababu ni mamlaka kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi kama ya Barabara ya Chalinze – Morogoro sasa ni miaka mitano tunaimba *PPP*. Sasa, kama barabara ile mpaka leo inashindwa kutekelezeka kwa mfumo wa *PPP*; maana ningekuwa na fedha mimi ningeijenga, inalipa; tutaweza barabara za mbali? kwa hiyo, niiombe sana Serikali ituletee mrejesho wa yale tuliyokubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Adonis Alfred, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

MHE. ADONIS A. BITEGEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza ninaanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyotoa msukumo mkubwa sana katika utengaji wa fedha kushuka katika bajeti, pia katika usimamizi wa rasilimali za Serikali ili kufikia malengo kusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hizi nyaraka ambazo zimewasilishwa, ule Mwongozo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali katika kipindi cha kati. Pia, nimepitia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba hizi nyaraka pamoja na yale Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali katika mpango wa kati zimeandaliwa kwa ufanisi mzuri kabisa. Ninaipongeza sana Serikali na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa jinsi walivyoandaa hizi nyaraka. Kwa upande wangu nitakuwa tu ninatoa msisitizo na maboresho katika sehemu ambazo ninaona kwamba zinahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Mpango ambao unapendekezwa wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2027/2028, umeweka mkazo mkubwa sana katika kuongeza tija, thamani ya

uzalishaji, kuimarisha ushindani wa bidhaa na huduma, na kuchochea uwekezaji wa ndani na nje, kuongeza ushiriki wa sekta binafsi na kuboresha huduma za kijamii na ustawi wa wananchi. Hapa ninajaribu kutoa msisitizo kwa sababu mchango wangu utakuwa unaangalia hapo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Ninaanza kuchangia zaidi kwenye masuala ya Bima ya Afya kwa Wote. Nimesoma mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo, ninadhani, licha ya kutoa kipaumbele katika Bima ya Afya kwa Wote, hasa utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ninadhani pia mkazo mkubwa ungepelekwa katika kuona ni namna gani tunaweza kuimarisha vyanzo vya fedha vya kugharimia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani hili suala ni la msingi sana. Ukiangalia nchi nyingi sana ambazo zimetekeleza Bima ya Afya kwa Wote, hasa za Afrika, zimekuwa na changamoto katika hilo eneo, kuona kwamba zinapata fedha za kutosha za kugharimia Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona awamu ya kwanza ya kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote, imeisha ambapo tumefanikiwa kwa 72%. Walengwa walikuwa kama kaya 278,000 lakini kaya 198,000 zimeweza kufikiwa, ambayo ni 72%. Kwa hiyo, kuna haja huko mbele tunavyoendelea katika awamu ya pili ambapo kaya 625,000 zitaandikishwa, kwanza tukahamasishe uandikishaji, kutoa elimu ya umuhimu wa wananchi kujiandikisha katika Bima ya Afya kwa Wote, lakini pia kuona namna gani tunaweza kuongeza vyanzo vya kugharamia Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, hasa kwenye zile kaya ambazo hazina uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa sababu hili ni eneo pekee ambalo pengine Serikali inabidi iangalie sana. Ninajua pia ipo mipango, vipo vyanzo vimebainishwa kama ule mfuko wa udhamini wa UKIMWI ambao umechangia 30% katika kugharamia Bima ya Afya kwa Wote katika kaya ya maskini, pia kodi kwenye vileo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji sana kuona ni kwa namna gani tunaweza kuimarisha vyanzo ambavyo siyo vya kikodi, hasa kupitia bima ya afya, kuona kwamba inawekeza zaidi katika vyanzo mbalimbali vya kukuza mapato yake na pia ikiwezekana basi kuingia katika masoko ya mitaji ili kukusanya zaidi fedha za kugharamia Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la msingi ambalo ningependa kusisitizia hapa ni suala la kuimarisha sekta ya viwanda. Ninafahamu kuwa Serikali katika Mpango huu wa mwaka 2027/2028 imejitahidi sana kuweka afua mbalimbali na mapendekezo ya kuimarisha namna bora ya kuvutia uwekezaji. Ningejielekeza zaidi katika upande wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya, yaani dawa na vifaatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kabisa na ninapongeza sana jitihada za Serikali kupitia Wizara ya Afya ya kuanzisha kongani za viwanda na kuvutia pia uwekezaji. Nimeona kwamba kusudio au lengo kubwa ni kuona kwamba ikifika mwaka 2028, basi angalau tumefikia 20% ya kuongeza zaidi kile ambacho tunacho katika kumudu mahitaji ya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna 20%, lakini ninadhani mpaka mwaka 2028 tutafika hata 40%. Basi tunahitaji jitihada za makusudi kabisa kuona kwamba tunavutia zaidi uwekezaji katika hili eneo. Moja, ni kuwa na vivutio vikubwa zaidi vya kikodi na visivyokuwa vya kikodi, ambavyo ni shindani zaidi ya wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia mojawapo ya kuweza kusaidia sana katika sekta hii ni kuona kwamba kwa vile viwanda vya dawa vya hapa nchini ambavyo tunahisi vimeweza kufikia uwezo wa kuzalisha dawa hapa nchini, basi zile dawa zao zipewe kipaumbele katika zabuni za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwenye upande wa dawa za maji za tiba, Serikali imetoa kipaumbele kwamba Bohari ya Taifa ya Dawa *(MSD)* ichukue kutoka katika vyanzo vya ndani. Basi vilevile, tupanue pia wigo, kuna viwanda vya dawa hapa nchini ninahisi vina uwezo kama dawa za *Paracetamol*, na

nyinginezo basi tuweke msisitizo kwamba hizi dawa zitakuwa zinatoka hapa ndani zaidi ili kukuza uwezo na ukwasi wa viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la msingi ambalo ninapenda kulizungumza ni suala la sekta ya uvuvi. Kwa upande wa sekta ya uvuvi tumeona Serikali ilivyojaribu kuweka afua mbalimbali katika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ni kuhamasisha ufugaji mkubwa wa vizimba vya Samaki, na pia kuna haja ya kuimarisha uzalishaji mkubwa wa vifaranga vya samaki, chakula cha samaki na vilevile kuhamasisha uwepo wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya bahari au maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la msingi ninaloona nilisisitize ni kwamba nimeona katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2027/2028 jitihada za Serikali katika kuimarisha sekta ya uvuvi ili ichangie katika pato la Taifa kwa 3.5%. Ninadhani kuna haja kubwa sana ya kuona kwamba ule mkakati wa Serikali au dhima ya Serikali ya kuanzisha mamlaka ya udhibiti ya rasilimali za bahari na maziwa, basi unaanza kutekelezwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati mwafaka sasa hivi wakati tumejipanga zaidi katika Uchumi wa Buluu tuone kwa namna gani tunaweza kuwa na mamlaka ambayo itakuwa inadhibiti rasilimali za bahari hasa katika uvuvi ambao unafanyika katika bahari na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho, ni suala la kilimo. Kilimo kimezungumziwa hapa kwamba ndio uti wa mgongo wa Taifa na kimsingi ndio ambao unategemewa zaidi katika kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na maeneo mawili ambayo pengine ningetoa msisitizo zaidi. Eneo la kwanza, kilimo kikubwa cha vitalu *(block farming)*. Ninahisi kwamba pengine pale tukiwekeza vizuri katika kilimo cha biashara kikubwa zaidi

cha *block farming*, kitaweza kuvutia zaidi uwekezaji mkubwa lakini pia wakulima wetu wataenda kuungana katika vikundi vidogo na kufaidika katika kilimo hicho kikubwa cha *block farming*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ni kitu cha msingi sana ambacho kinapaswa kusisitizwa hapa ni kwamba, ni kwenye upande wa kilimo cha mkataba. Mbali na *block farming* lakini kilimo cha mkataba ili kuona namna gani kwamba wakulima wadogowadogo wanafaidika kwa kuingia mikataba na kampuni kubwa ambazo ni za kilimo ambapo watafaidika kwa upande wa utaalamu na kwa pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo pengine ninaomba hapa nilisisitize ni suala la mashirika ya umma. Kumekuwa na vikao vya Msajili wa Hazina na Wakuu wa Taasisi za Umma mwaka 2025 na mwaka 2026. Ninadhani sasa hivi ni wakati mwafaka kuweka msisitizo zaidi mashirika ya umma yawekeze katika kufanya biashara zaidi na kupata faida. Kwanza, kuingia katika masoko ya mitaji kwa kuuza hati fungani, lakini ikiwezekana pia na kuweka dhamana kwa ajili ya kuvutia zaidi uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishie hapo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas.

MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia mpango wetu huu uliopo mbele yetu. Ninaomba nitaje mambo machache. La kwanza, nipongeze mpango wetu mzuri ambao umeandaliwa. Hakika umeandaliwa kwa ustadi mkubwa sana na tunaipongeza Wizara pamoja na wataalamu wote ambao wameshiriki katika kuuandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninapenda kusema kwamba pamoja na mpango mzuri, mpango wetu huu unahitaji fedha ili uweze kutekelezwa na kuweza kufikia matokeo ambayo tunayatarajia ifikapo 2050, lakini pale ambapo tunajadili kwa

maana ya mwaka wa fedha unaokuja, tutahitaji fedha ili kuweza kuutekeleza na kufikia malengo ambayo tunayatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunahitaji uongozi thabiti ambao utahakikisha kwamba tunasimamia yale ambayo tumeyapanga yaweze kutekelezwa kwa kutumia viashiria vilivyopangwa na kuhakikisha kwamba vinapimwa na kuripotiwa ili kujua maeneo ambayo tumeyafikia na maeneo ambayo hatujayafikia ili kuweza kufanyiwa utaratibu wa utekelezaji wake. Hayo yatatufikisha katika utekelezaji mzuri wa matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mpango wetu huu kama Watanzania, tunahitaji watu ambao wana afya njema na ambao wataweza kushiriki katika utekelezaji wa mpango wetu wa maendeleo katika sekta mbalimbali. Ili tuwe na watu wenye afya njema, tunahitaji kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara yetu ya Afya kufanya uzinduzi wa bima ya afya kwa wananchi wote, na hii ni utekelezaji wa Sera ya Chama cha Mapinduzi. Hakika tumpeni maua yake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na pia na Wizara yetu ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Wabunge watuunge mkono katika majimbo yao kuweza kuwahamasisha wananchi kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote katika kuhakikisha wananchi wetu wanaweza kupata matibabu pale ambapo wanahitaji ili wawe na afya njema na waweze kushiriki kwenye shughuli zetu za uzalishaji na ujenzi wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo matatu ambayo ninapenda kuyasema. Ili tutekeleze mpango huu, tuna mambo mengi sana ambayo yameandikwa na yameainishwa na hakika ni ya muhimu sana. Pia yapo mambo matatu ambayo pengine mimi nitaweza kuelekeza hoja zangu hapo. Moja, tunahitaji miundombinu, mfano tunahitaji barabara na reli ambayo inafanya kazi kama tulivyoona *SGR* yetu, na reli nyingine ya

kawaida inayoenda Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati na pia na Reli ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji bandari ambayo Serikali imefanya uwekezaji mkubwa na sasa tunaona bandari imeanza kuzidiwa kwa kuona kwamba sasa barabara haziwezi kupokea mzigo ambao bandari inaingiza nchini. Kwa hiyo, tunahitaji kuona namna ya kuboresha barabara zetu ili kasi ambayo ipo bandarini iendane sawasawa na kasi ya uwepo wa barabara kupokea mizigo inayoingia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uboreshaji wa viwanja vya ndege, navyo pia ni vya muhimu. Vilevile, bila kusahau usafiri wa majini kwa ajili ya bahari na maziwa yetu tuliyonayo. Hiyo ni miundombinu na mimi ninapenda kusema katika miundombinu nitajikita kwenye eneo la barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunahitaji maji. Maji ni muhimu sana kwa matumizi yetu ya majumbani, viwandani, kwenye kilimo lakini na pia katika sekta nyingine. Hilo nalo ni eneo muhimu sana katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza mpango wetu huu wa maendeleo. Jambo la mwisho, tunahitaji nishati ya umeme na mafuta, nami nitajikita katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la barabara, tunajua kwamba hii ni nguzo muhimu sana. Tukitaka kwenda mashambani tunahitaji barabara, tukitaka kwenda viwandani tunahitaji barabara, tukitaka kutoa bidhaa kutoka viwandani kwenda sokoni tunahitaji barabara, na tukitaka kutoa malighafi mashambani na kwenye maeneo yalikozalishwa iwe ni madini iwe ni nini tunahitaji barabara zinazopitika majira yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tuna barabara zetu za Taifa ambazo zinaunganisha mikoa na tuna barabara zetu katika ngazi ya halmashauri ambazo zinaunganisha vijiji, kata pamoja na tarafa zetu. Barabara zetu zina changamoto na bila kufanya uwekezaji wa makusudi katika eneo la barabara, mpango huu hautatekelezwa ipasavyo kwa sababu barabara ndiyo nguzo

muhimu sana, ndiyo kiunganishi muhimu sana cha uchumi wetu na cha kuhakikisha kwamba tunatekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba katika eneo hili tunaona barabara zetu zinazounganisha mikoa. Ukiangalia barabara ya Arusha, Babati, Katesh, kwenda Singida, tunaishukuru Serikali imetoa shilingi bilioni 31 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ule. Tunaipongeza Serikali, lakini bado tuna barabara nyingine ambazo bado zinalalamikiwa kwenda kusini, kwenda kanda za juu magharibi, na pia kwenda kanda ya ziwa, kwa maana ya barabara ya Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma - Tabora, mpaka Mwanza lakini zinazounganisha na Mikoa ya Kigoma na upande wa Mbeya pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado barabara hizi zimezidiwa, haziwezi kusafirisha mizigo kutoka bandarini, na pia kutoka katika nchi za jirani na mikoa yetu kwenda bandarini, vilevile kwenda kwenye mahitaji ya wananchi. Kwa hiyo, tunahitaji uwekezaji wa makusudi, na tunahitaji kupata mitaji ya makusudi ili tuweze kujenga barabara zetu tuziimarishe na vilevile tuzipanue ili ziendane na uwezo wa uchumi wetu na ukuaji wa uchumi wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunahitaji kutazama, je, tupate wapi mitaji? Tunahitaji Wizara ya Mipango, Wizara ya Fedha ituletee mipango hiyo kama Wabunge ili tuone namna ya kupata fedha kwa ajili ya kupanua barabara zetu ziweze kupitika na uchumi wetu ukue kwa kasi kubwa ili twende na ushindani wa kanda yetu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *PPP* ni suala la muhimu sana. Suala la ushirikiano wa sekta ya umma na sekta binafsi ni muhimu sana. Tuangalie Mheshimiwa Rais ameweza kutekeleza mradi wa *SGR*. Angalia ile *SGR* inayokwenda kwa kasi ambayo inakwenda masaa matatu na robo kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo inajaa na huwezi kupata nafasi siku mbili kabla. Maana yake wananchi wanahitaji mfumo fanisi

wa kuwawezesha kiuchumi na siyo kwamba hawana fedha. Kwa hiyo, tunaomba tuunge mkono uwekezaji wa sekta binafsi katika eneo la barabara ili tupate barabara nzuri na imara kwa ajili ya kubeba uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiogope na tuwaombe watendaji wetu wa Serikali wasiwe na kigugumizi katika kuharakisha ushirikiano wa *PPP*. Wasiwe na kigugumizi katika maamuzi na wasiwe na kigugumizi pia katika kutoa mapendekezo kwa wakati ili uchumi wetu ukue kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara zetu za halmashauri ambako hakika zinaratibiwa na kukarabatiwa na *TARURA*, nazo zina changamoto kubwa. Tulipitisha bajeti hapa, tunaomba sana barabara hizi zikatengenezwe na zipewe fedha za kutosha. Vivyo hivyo tuweke uwekezaji wa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuweka pendekezo moja, tuna barabara zetu kule vijijini. Unakuta barabara ya kilometa 60, sehemu iliyoharibika ni kilometa tano au sita lakini inakwenda kukwanguliwa barabara nzima. Tunatumia fedha ambazo zingeweza kukarabati maeneo zaidi ya 20 kwenye barabara ya kilometa 50 ambao ukarabati unahitaji kilometa tano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuokoa fedha za umma ili tuone thamani ya fedha kwa ajili ya barabara zetu. Ninapenda kutaja eneo la maji. Kwenye eneo la maji, tunahitaji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, tunahitaji kwa ajili ya matumizi ya migahawani na kwenye mahoteli, tunahitaji pia kwa ajili ya mashambani na tunahitaji pia kwenye viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba miradi ambayo Serikali imewekeza fedha nyingi. Tunatoa maji kutoka Ziwa Victoria tunaleta mpaka Dodoma. Tunahitaji maji kwa ajili ya viwandani, na vilevile tunahitaji kwa ajili ya matumizi ya mashamba. Tunaomba miradi hii ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika halmashauri zetu pia tuna miradi ambayo inaendelea. Mingi imekwama, ina miaka miwili, mingine ina miaka mitatu. Maji haya ndiyo *drive* kubwa sana katika kutekeleza mpango huu. Viwanda vinahitaji maji, umwagiliaji unahitaji maji, lakini pia matumizi ya majumbani yanahitaji maji. Ninaomba miradi hii ikamilike. Kama katika halmashauri yangu, nina Mradi wa Dambia ambao ni mkubwa, ninaomba tuukamilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie hoja zangu mbili za mwisho. Nishati ya umeme inahitajika sana, lakini umeme unaohitajika uwe wa gharama nafuu, na vilevile uwe wa uhakika. Tunampongeza Mheshimiwa Rais, tumeweza kufungua Bwawa letu la Mwalimu Nyerere na tunazalisha umeme wa kutosha, lakini bado gharama za uunganishaji ni kubwa sana, hasa kwenye eneo la *three phase* ambako ndiyo tunataka ku-*encourage* viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe Wizara yetu ya Nishati lakini pia kushikamana na Wizara ya Uwekezaji ione namna ya kuweka utaratibu wa kukopesha wale wanaotaka kuunganisha umeme wa uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo ili kusiwe na gharama kubwa sana. Hii itazalisha ajira nyingi na pia itaongeza tija na itapunguza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru sana, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, ajiandae Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu kwa uchache kwenye hoja hii ambayo ipo mbele yetu. Nchi yetu inapiga hatua za maendeleo na hatua zilizopigwa siyo kidogo, ni kubwa na tunaipongeza sana Serikali yetu kwa hatua zote ambazo inaendelea nazo. Nchi yetu imepiga hatua kwenye

uchumi jumla. Pato la Taifa limeongezeka, lakini pato la kila Mtanzania nalo limeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei umedhibitiwa vizuri, wastani wake siyo mbaya, ni mzuri kiasi cha kuiwezesha nchi kuendelea kupiga hatua za maendeleo makubwa zaidi. Hata hivyo, tuna fedha za kigeni nyingi za kutosha kuweza kuendesha nchi yetu kwa muda wa miezi zaidi ya minne. Pia kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, tumepata taarifa umaskini umeweza kupungua kwa Watanzania. Sasa hatuwezi kujidharau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tumpongeze Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya kwa Taifa letu na ndiyo maana tunapiga hatua za maendeleo namna hii. Ninajua na ninatambua kwamba huko mitaani kuna watu wanapitapita na kusema nchi hii oooh miaka 60 na kitu hiki hakipo wala hiki hakipo, lakini hawataji pia mambo ambayo hayakuwapo wakati tunapata uhuru na sasa yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maendeleo makubwa ambayo anaendelea kuyafanya kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hiyo, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji, ndugu yangu na mwalimu wangu katika siasa ameweza kutuletea mpango mzuri ambao umetoholewa kwenye dira yetu ya maendeleo na pia mpango wa nne wa maendeleo wa muda wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira yetu ya maendeleo ya mwaka 2050 inaonesha tunaelekea wapi na tutafikaje huko 2050. Ninachukua nafasi hii kumshukuru tena Mheshimiwa Rais, maana huo ndiyo uongozi kwamba lazima utoe dira mwelekeo wa watu unaowaongoza, mnataka mfike wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hilo halina mashaka na Watanzania na Waheshimiwa Wabunge sasa hivi tunaelewa

kwamba tunaelekea wapi na ndiyo maana mwelekeo huo umegawanywa kwenye vipindi vya miaka mitano. Sasa tuko kwenye mwaka wa kwanza wa kutekeleza mpango wa kati wa miaka mitano mpaka 2030/2031 na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji ametuletea mpango huu. Haya ni mapendekezo ambayo yanawekwa mbele yetu ili sisi tutoe mambo yanayotakiwa, yaboreshwe kabla hajauleta mpango wenyewe mwezi Machi mwakani 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo siku zote tunafahamu, mipango iliyowekwa mbele yetu ni mizuri na inafaa na ikitekelezwa inaweza ikatupeleka kwenye dira ya 2050. Sasa ninapenda nizungumze mambo mawili tu kwenye mpango huu ambao uko mbele yetu. Jambo la kwanza, ninataka nizungumze mpango wa kupata pesa ukoje, lakini na jambo la pili nitazungumza juu ya kupunguza matumizi ili kwamba tuweze kufika huko tunakotaka tufike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mipango hii tunayoijadili tutakayoipitisha iweze kutekelezwa vizuri, lazima tuwe na mapato. Tunamshukuru tena Mheshimiwa Rais amesimamia upatikanaji wa mapato kwa muda wa vipindi vya miaka miwili mfululizo mapato yetu ambayo tunapitisha hapa Bungeni ili yakusanywe ili mipango yetu iweze kutekelezwa, yameenda vizuri; mpaka mpango ulioisha wa mwaka 2025/2026 ulioisha Juni, tumekusanya fedha kiwango cha kutosha zaidi ya 98% ya mapato tuliyokuwa tunategemea yalipatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana na kuimarika kwa wakusanya mapato *TRA* na maeneo mengine, lakini bado tunahitaji tuongeze mapato yetu ili kuweza kukamilisha mipango iliyoko kwenye dira na iliyoko kwenye mpango wetu ambao tunaujadili hapa. Moja ya eneo ambalo halijapewa kipaumbele ni eneo la *carbon credit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili ni eneo ambalo linaweza likatupatia fedha nyingi. Ninatambua limetupa fedha kidogo lakini bado kuna maeneo mengi ambayo hayajafanyiwa tathmini

yakaweza kutupa fedha za kutosha kuweza kuendesha mambo yetu kwenye baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu iliyoko *TFS* haifanyiwa tathmini pamoja na misitu mingi na maeneo mengine ambayo yako kwa nchi yetu yanayoweza yakatupa *credit* na tukapata pesa kwenye eneo hili. Sasa ni muhimu kwa Serikali kufanya juu chini ili misitu yetu iliyoko *TFS* na maeneo mengine tuwezeshe kituo chetu cha *carbon* kiweze kufanya tathmini na tuweze kuona ni kwa namna gani tunaweza kupata mapato kutoka kwenye hili eneo. Mapato mengi ya kutosha yapo kwenye eneo hili. Hata hivyo, bado kama Serikali hatujafanya jitihada ya kutosha kuweza kukusanya mapato kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo hatujalitumia sawasawa ni eneo la maduhuli. Maduhuli ya Serikali kwenye taasisi za Serikali, kwenye halmashauri zetu bado hatujatumia vizuri kwa sababu bado kuna changamoto nyingi juu ya ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri zetu, kwenye taasisi zetu na hata kwenye Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinazoletwa mbele yetu zinaonyesha ni kwa namna gani malengo hayakuweza kufikiwa kwenye eneo hili. Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali kuangalia upya malengo yanayowekwa na kusimamia vizuri watu walioko kwenye taasisi hizi ili waweze kukusanya mapato ya Serikali yaweze kutusaidia kuelekea kutimiza malengo yetu ya mwaka 2020 - 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni baadhi ya maeneo tu machache ambayo tunaweza kuongeza mapato yetu. Sasa kwa sababu kengele inalia kwa haraka sana, niende kwenye eneo lingine kuhusu namna gani tunaweza kubana matumizi yetu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Ninaona kengele inalia.

MWENYEKITI: Malizia Mheshimiwa.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Basi namalizia kwa kusema, tukipata fedha kama ambavyo tunapata fedha leo, lazima Serikali ikubali sasa kubana matumizi. Hatuwezi kuendelea na raha zilezile wakati tumeweka malengo makubwa kwenye Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Serikali ikubali kubana matumizi. Serikali ihamie Dodoma yote kwa ujumla. Badala ya kuwa na ofisi mbili, Dar es Salaam na Dodoma, lazima tukubali kubana matumizi. Mheshimiwa Rais na viongozi wetu wameonesha njia na nia ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru basi tutapata nafasi wakati mwingine tunaweza kueleza. Ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano, ajiandae Mheshimiwa Isaya Ngurumi Moses.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama ambaye anajitahidi kuhakikisha tabasamu ya Watanzania inadumu. Ninaipongeza Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Waziri Mheshimiwa Profesa Kitila, Naibu wake na watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na waliotangulia katika wachangiaji na katika kuungana nao ni sehemu ile ya kusisitiza suala la sheria kwa mpango huu kwa dira hii ili iweze kudumu kwa sababu hiyo ndiyo tunu ya kuipa nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mheshimiwa Prof. Kitila imepewa jukumu kubwa la kutafsiri ndoto ya Watanzania kama ambavyo Nabii Yusuf alitafsiri ndoto ya Wanamisri mpaka Mfalme

wa Misri, Farao (Waarabu wanamwita Firaun) akamsifia akiwaambia watumwa wake, tupate wapi sasa mtu kama huyu mwenye roho ya Mungu ndani yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari za Nabii Yusuf ni nyingi, lakini katika *Quran* Sura ya 12 ambayo ndiyo Surat Yusuf, Mungu anaeleza habari hizi za Yusuf kwamba *"taz-ra'oo-na sab-'a si-nee-na da-'a-baa."* Ninyi mtavuna miaka saba mazao bila shida. *"Fa-maa ha-sat-tum fa-dha-roo-hu fee sum-bu-li-hee il-laa qa-lee-lam mim-maa ta'-ku-loon."* Mtakapokuwa mmevuna jitahidini sana kuweka akiba isipokuwa kidogo tu kwa ajili ya kula. *"Thum-ma ya'-tee mim ba'-di dhaa-li-ka sab-'un shi-daa-duy ya'-kul-na maa qad-dam-tum la-hun-na il-laa qa-lee-lam mim-maa tuh-si-noon."* Baada ya hapo itakuja miaka saba ya shida sana, itakuja miaka saba ya shida sana kwa maana miaka saba ya njaa, *"yaakuluna maakaddamtum lakunna illa kaliilan ma tukhsinuun."* Yote mliyoyaweka katika maghala yataisha isipokuwa kidogo katika mbegu. Akasema *"Thum-ma ya'-tee mim ba'-di dhaa-li-ka 'aa-mun fee-hi yu-ghaa-thun naa-su wa-fee-hi ya'-si-roon"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuja mwaka mmoja watu watapata mazao mengi, mazao ya vyakula na matunda. Hii dira ya Nabii Yusuf ilikuwa ya miaka 15, lakini iliyowazezesha mpaka nchi jirani za Kanani zikaweza kufaidi. Kwa hiyo, kwa hii ya kwetu ya miaka 50 inahitaji kulindwa vizuri sana. Kwa sababu muda ni kidogo mengine nitaandika, lakini nisitize maeneo machache kwa maana ya kuimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni teknolojia ya kisasa, ambayo inatakiwa iambatane na mifumo ya kidijitali pamoja na akiliunde au *artificial intelligence*. Nini lengo? Lengo letu iwafikie wale wakulima wadogo, wawezeshaji, na yule mtu wa vijijini hata aliyeko Bumbuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwekeze katika miradi ya kilimo cha umwagiliaji, kilimo ambacho ni cha uhakika kwa muda wote wa mwaka, kitakachokuwa kinabadilika ni mazao gani yapandwe mwezi gani kulingana na *crop calendar,* lakini siyo suala la uhitaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwekeze katika uhifadhi wa maji ya kutosha ambayo yataweza kuendana na mabadiliko ya tabianchi ili yasiweze kuuyumbisha mpango wetu wa muda mrefu. Katika elimu ya maji huwa kuna maghala ya maji ukiacha maghala ya chakula, na maghala haya ni mabwawa makubwa ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kuendelea kuitafsiri ndoto, mambo haya ya kuweka msisitizo katika maeneo hayo miradi mikubwa ambayo itakuwa inahusu nishati, viwanda lakini na miundombinu iendane sambamba na uzalishaji wa mazao ya chakula na malighafi kwa ajili ya viwanda mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yaendane sambamba na maghala ya kisasa pamoja na majokofu *(cold rooms)* kwa sababu katika hasara tunayoipata Tanzania, ni mazao ya mbogamboga na matunda ambayo yanajenga mwili sana. Ninatoa mfano Wilaya ya Lushoto Mkoa wa Tanga na Muheza, na Mikoa ya Mbeya na Iringa pamoja na Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwe na maeneo ambayo ni *strategic areas* kwa sababu mazao ya matunda yana tabia kitakwimu huenda ukapoteza hata 40% ya kuoza. Kwa hiyo, itakapofika hizi *cold rooms* tutaokoa sana na hapa afya ya Mtanzania itatengamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ningesisitiza iimarishe usimamizi wa fedha za umma, lakini pia ufuatiliaji wa miradi na utawanyaji wa fedha za miradi kwa wakati. Hii itazuia kuchelewesha miradi, itazuia gharama zisiongezeke kwa sababu mradi ukichelewa, gharama zina kawaida ya kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makundi maalum ya vijana, wanawake na wenye ulemavu, niishauri Serikali, makundi haya yawezeshwe kupitia mafunzo kupitia mitaji, kupitia masoko teknolojia na huduma za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na waliotangulia katika suala la barabara. Ziko barabara zetu za kimkakati za Dar es

Salaam, Morogoro, Mbeya Iringa Mbeya hizi ni barabara ambazo ni muhimu sana, zijengwe katika mfumo wa njia nne na yale magari ambayo hayana spidi kubwa ikiwepo malori, yawekewe leni za pembeni wakiwepo bajaji maguta hapa katikati watu wanaowahi wawekezaji Mbeya na Iringa kwenda kufanya biashara wasichelewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni pamoja na barabara ya Chalinze – Tanga – Moshi – Arusha na Tanga mjini pia. Barabara ya Tanga Mjini kuelekea Arusha imeanza kuzidiwa kwa uwekezaji mkubwa wa Bandari ya Tanga. Tunaishukuru Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuchangia, kuna eneo ambalo bado hatujafanya vizuri, eneo la makaa ya mawe. Eneo hili wenzetu wa Zambia sasa wanazalisha ile gesi ambayo inatumika kutengeneza mbolea ya *urea*. Kupitia makaa ya mawe, tunaweza tukazalisha aina mbalimbali za lami ambazo zingeweza kusaidia ujenzi wa barabara zetu. Sasa hapa tunatakiwa twende spidi, ifike mahali sasa mambo mengi yawe yanapatikana ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuitafsiri ndoto hii, Mheshimiwa Prof. Kitila katika sekta yake ana jambo kubwa la kufanya. Miongoni mwa mambo muhimu, ni kuunganisha barabara, ni ujenzi wa barabara zinazounganisha maeneo ya uwekezaji, na masoko ambako bidhaa zitaelekea; maeneo haya lazima yapo mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mheshimiwa Prof. Kitila anayosimamia ni Wizara Mtambuka, haiwezi ikaenda peke yake bila Wizara nyingine. Nishauri, kwa kuwa kuna tatizo kubwa kwa baadhi ya maeneo, mifumo yetu kutosomeka, ni wakati sasa wa kulazimisha kila mfumo usomane na mwenzake ili tuweze kufikia malengo ya ndoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, ninaunga mkono hoja. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Issa Mngurumi Moses, ajiandae Mheshimiwa Ado Shaibu Ado.

MHE. ISAYA M. MOSES: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ila kwa jina ninaitwa Isaya Mngurumi Moses. Siyo Issa, ni Isaya. Ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo kwa kazi kubwa aliyoifanya. Kwa kweli amekuwa ni mwalimu mzuri sana, ametufikisha mahali pazuri, nimshukuru sana yeye binafsi, na timu yake yote katika ile Wizara kwa kazi wanayoifanya. Pia, niishukuru Wizara ya Fedha, nikianza na Mheshimiwa Waziri na watumishi wake wote wa Wizara ya Fedha. Pia, ninamshukuru Mwenyekiti wa Bajeti, na yeye jana ameweka *summary* yake pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala tulilonalo sasa hivi ni mapendekezo ya mpango wa mwaka 2027/2028 lakini kubwa zaidi hapa ni malengo ya kufikia Dira ya 2050. Ipo haja sasa kwa Watanzania kupitishwa na kuelimishwa, yaani *ipite capacity building,* tuongee kitu kimoja, kwa sababu inawezekana Bunge linaongea, na wachache wanaongea lakini Watanzania hawajui nini maana ya Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ya kufanya *capacity building* kwa wananchi, kwa sababu isije ikafikia mahali tunaimba wachache, wengine tunawaacha. Kwa nini ninasema hivyo? Ninasema hivyo kwa sababu, nikiwa kwenye ziara, yapo mambo niliulizwa, nini maana ya Dira ya 2050?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikabidi nijibu, maana uzuri na mimi nina *element* ya uchumi, nikalizungumza vizuri. Dira yetu tunakotaka kwenda 2050 kiufupi *(simple definition)* ni maisha bora kwa kila Mtanzania. Watanzania wawe na maisha mazuri, maisha bora. Ndiyo hiyo hali tunayoitafuta sasa hivi. Nikawaambia, pato la mtu mmoja tunategemea lifike dola 7,000 na pato la Taifa lifike dola trilioni moja. Tunafikaje huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawaambia kufika kwenyewe ni kwamba, iko mipango ambayo tunaifanya. Kwanza, kuhakikisha kwamba tuna mipango mizuri ya kuboresha kilimo, mifugo, ujenzi na miundombinu, madini, utalii, masuala ya viwanda na biashara. Tunaboreshaje kilimo? Kilimo tunakiboresha kwa kuwa na kilimo cha umwagiliaji, maana yake tuwe na maji, tusitegemee mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, umwagiliaji wenyewe unakuwaje? Nikawaeleza kuwa tutatumia mito, sehemu yenye mito, tutachimba mabwawa makubwa ili tufikie kwenye lengo letu hilo. Hapa sasa ikawa shida, maana jimboni kwangu kule kuna bwawa ambalo linatamkwa karibu miaka saba la shilingi bilioni 106, liko Kijiji cha Ngomai pale. Mpaka leo lile bwawa halijafanyiwa chochote kile, lipo pale, tunazungumza tu, lakini hakuna kinachoendelea. Hilo ndilo lilikuwa mwarobaini wa kufanya mambo ya umwagiliaji yaende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwangu tu, na sehemu nyingine, kwenye suala la mabwawa Wizara ya Kilimo ninaomba mjipime kwenye hilo suala. Maana mmekuwa mnaandika sana, lakini utekelezaji umekuwa ni kidogo. Kwa mfano, pale kwangu, tayari watu wameshatoa eneo kwamba bwawa litakuja na watu walitegemea kwamba mvua zinazokuja hizi za *El-Nino,* tutatumia hilo bwawa, maji yatajaa, lakini mpaka sasa hivi ni kitendawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawaeleza kwenye kilimo kwamba tutaboresha mambo ya visima vya maji. Tutachimba visima ili mambo yaweze kwenda vizuri. Bado kuna swali likaja kama unazungumzia masuala ya kilimo cha umwagiliaji cha mambwawa ya visima, mwaka huu mvua imenyesha vizuri, wananchi wamepata mazao ya kutosha. Yaani ukipita kule kila nyumba sasa hivi mazao ni ya kutosha. Siyo kwangu tu, na sehemu nyingine lakini tatizo ni bei. Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji waangalie wale watu. Wale watu wanategemea kilimo na ndiyo maisha yao, lakini bei ya mazao imeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilo moja ya mahindi sasa hivi ni shilingi 320 mpaka shilingi 400 kwa kilo. Sasa ukiangalia mtu akiuza anapata hasara. Mahindi ni mengi, lakini Serikali mpaka sasa hivi

iko kimya kuhusu suala la bei, haisemi chochote. Ukienda kule jimboni na hilo ndilo jambo linalozungumzwa mpaka unaogopa. Kweli watu wamelima, mazao yamepatikana lakini bei hakuna. Sasa, nini shida? Sijui *NFRA* haionekani, sijui tumefunga mipaka, tumefanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anahitimisha, ninaomba alizungumzie suala la bei ya mahindi, kwa sababu limekuwa ni shida na watu wanasema unataka tufike kwenye dola 7,000, lakini sasa hivi tuna dola 1,200 mpaka dola 1,300, na bei ya mahindi imeshuka. Ina maana sasa hivi tunarudi nyuma, au tunakwenda mbele? Inaonekana wananchi sasa hivi wanarudi nyuma na wanategemea kilimo. Sasa ninashindwa kuelewa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tufanye mkakati wa kutosha wa kuhakikisha bei ya mazao, hasa bei ya mahindi inapanda. Wakanipa hesabu, bei ya kilo mbili za mahindi ni shilingi 18,000. Shamba la ekari moja linalimwa, na linapandwa kilo nane.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ISAYA M. MOSES: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya kwanza hiyo au ya mwisho?

MWENYEKITI: Ya kwanza Mheshimiwa.

MHE. ISAYA M. MOSES: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nimekuwa Mheshimiwa Profesa Muhongo kidogo, ninapiga *data* sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakaniambia kulima, mbegu ni shilingi 72,000. Ukiangalia mbegu bora ya shamba, kilo nane kwa ekari moja na ukiangalia pale kwa kilo mbili ni shilingi 72,000, bado hajalima. Kulima kwa trekta ni shilingi 20,000, ana palizi mbili; ya kwanza shilingi 20,000, na ya pili shilingi 20,000. Anarudisha mazao. Ukipiga hesabu ya gharama zote hizo unakuta ni kama shilingi 200,000 na kitu. Ukiangalia kwa sasa

kutokana na hali ya maji na kilimo na nini mkulima anavuna kidogo, kwa ekari moja unakuta anapata gunia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa gunia nne hazitoshi kwa sababu bado hatujawawekea mbinu ya kutoka. Tukienda kwenye kilimo cha umwagiliaji, mkulima huyo atapata gunia 40. Kwa hiyo, ukiangalia mkulima akienda kuuza sasa hivi mahindi yake, kwa kila gunia moja anapata hasara ya shilingi 60,000 ya hasara. Sasa unajiuliza, tunakwenda mbele, au tunarudi nyuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali itusaidie ili twende jimboni kule tuweze kuongelewa vizuri, kwa sababu sasa hivi ukienda jimboni kule watu wana mahindi mengi, lakini hayo mahindi hayauziki. Ninaiomba sana Serikali ifanye hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nikazungumzia suala ya ufugaji. Ufugaji mnafanya nini? Nikasema tutaboresha malisho, yatakuwa mazuri. Tutaboresha masuala ya maji, tutaboresha masuala ya migogoro ya ardhi kuhakikisha kwamba wanapimiwa maeneo yao, wakaniambia sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaenda suala la miundombinu, hapo sasa ndiyo ikawa shida. Miundombinu kama jana alizungumza Mheshimiwa Tabasamu, kwamba Kongwa yenyewe iliahidiwa barabara na ilisainiwa mkataba na shahidi wa ule mkataba alikuwa Mheshimiwa Rais toka mwaka 2021 mpaka leo hakuna hata tripu moja ya mchanga iliyokwenda pale. Hiyo barabara iliahidiwa itakuwa ni barabara ya lami ya kutoka *Kongwa Junction* – Kiteto - Simanjiro - Arusha kilometa 453 lakini mpaka leo pale kwenyewe Kongwa inakoanzia, hata tripu moja ya mchanga haijaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakaniuliza tunakwenda wapi, hayo unayoyazungumza ndiyo ya Dira ya 2050 kwa mtindo huu? Niwaombe sana, nimwombe sana Mheshimiwa Kadogosa aiangalie hiyo barabara, ni barabara ya uchumi inayotoka Arusha – Simanjiro - Kiteto mpaka Kongwa inaenda Mpwapwa - Kibakwe mpaka Iringa. Hiyo ni barabara ya Uchumi, lakini jana Mheshimiwa Tabasam hakuitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Kadogosa aiangalie hii barabara. Halafu tunamdhalilisha Rais. Rais alisimamia ule mkataba na watu walipiga picha, wanazo, kwamba Rais amesimamia huo mkataba, amekuwa shahidi, halafu barabara haitengenezeki, ina miaka zaidi ya saba, imekaa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mengi, lakini ninaona kengele zimelia na mimi ninaheshimu muda. Ninaomba tu niishie hapa, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, ajiandae Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa.

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa maoni yangu katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Nitatoa maoni yangu kwenye maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, nimetoka jimboni karibuni na kama mnavyofahamu, mabosi zetu sisi ni wananchi na katika kuzunguka kwangu mabosi wangu (Wananchi wa Tunduru) wameniambia, "Mheshimiwa Mbunge, acha kuzungumza unayotaka kuzungumza. Ajenda ni moja tu, tunataka hatma ya mgogoro wa wakulima na wafugaji." Kwa hiyo nitaanza na hilo, kwa sababu nisipoanza na hilo, mabosi wangu hawatanielewa hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma nyaraka ambazo zimewasilishwa kwetu, kama tulivyozoea kwenye miaka mingine iliyopita, imewekwa bayana kabisa kwamba katika pato la Taifa, kilimo kina nafasi ya kipekee lakini hata katika ajira imewekwa bayana kwamba kilimo kinaongoza. Kinachoendelea Jimboni kwangu Tunduru Kaskazini na katika maeneo mengi ya Lindi, Mtwara, na Pwani, kilimo kitarudi nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkutano uliopita, nikimwuliza swali Waziri Mkuu, nilitahadharisha kwamba kile kinachoendelea

Tunduru na Kusini kwa ujumla wake, kama hatua madhubuti hazitachukuliwa tutashuhudia maafa makubwa sana. Kwa masikitiko makubwa sana ninaomba kusema kwamba tangu nitahadharishe katika mkutano uliopita mpaka leo kwa Tunduru peke yake, tumeshazika watu tisa katika muda huu mfupi…

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Taarifa.

TAARIFA

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninampongeza Mheshimiwa Ado kwa mchango wake, ninaomba kutoa taarifa Bungeni kwamba, Jumatatu iliyopita Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya kikao katika ofisi yake na Wizara nane, wakiwepo Wabunge wote wa Mkoa wa Ruvuma, waliweza kufika na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, ametoa maelekezo kufuatilia jambo hilo ambalo haliko Ruvuma peke yake, liko katika na mikoa mingine na maelekezo hayo yanaendelea kufuatiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba machafuko yanayoendelea katika maeneo yote nchini yakome na kuanzia kikao chake, Wakuu wa Mikoa wahakikishe hakuna mwananchi anayeumizwa. Pia, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema atafanya ziara akitoka Urusi kwenda kuzungumza na wananchi wa Wilaya ya Tunduru pamoja na Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ado, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea kwa sababu alichokisema Waziri, Mheshimiwa Dkt. Bashiru ndicho ninachokisema. Kwanza, anakiri kwamba hali ni mbaya, ametumia lugha ya machafuko, maana yake hali ni mbaya. Kwa

hiyo, ninakubaliana naye. La pili, amesema iko *Intervention* ya Serikali ya Waziri Mkuu, ninakubaliana naye, lakini ninaona haitoshi, ni lazima kuweka rekodi sawa ndani ya Bunge, yale ni mashauriano nje ya Bunge. Ninaweka rekodi ili baadaye tuje tupimane sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema kwa kifupi kwa sababu Waziri mwenye dhamana pia amesema. Wakati nimeweka tahadhari yangu mbele ya Waziri Mkuu, Waziri Mkuu alitoa maelekezo mawili: agizo lake la kwanza lilikuwa ni kwamba Vyombo vya Ulinzi na Usalama visimamie sheria. Agizo lake la pili lilikuwa viongozi katika ngazi husika wasimamie mpango wa matumizi bora ya ardhi. Kwa masikitiko makubwa sana, maagizo yote yale mawili hayakutekelezwa ipasavyo. Ndiyo maana ninataka kuweka rekodi ndani ya Bunge kwamba, kuagiza ni jambo moja, lakini utekelezaji ni jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Dkt. Bashiru afuatilie nini kinaendelea Tunduru tangu Waziri Mkuu ameagiza? Kinachoendelea hivi sasa ni watu kuwageuza wafugaji kuwa *ATM*, kuwakusanya katika maeneo ambayo wako kinyume na sheria, kuwatoza fedha, halafu kuwaacha waendelee na maisha kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeiweka kwenye rekodi makusudi kwamba ni kweli tunaishukuru Serikali, imeona na tunamsubiri Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hamu. Ni vizuri maagizo yanayotolewa na Serikali yafuatiliwe kwa uzito mkubwa sana, la sivyo, tunaweza tukajikuta katika hali mbaya sana na malengo ambayo tunajiwekea katika mipango yetu ya mendeleo yasiweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni la kwanza na ninadhani kwa kufanya hivyo, mabosi wangu walionituma niseme ndani ya Bunge, wananchi wa Tunduru watakuwa wamefarijika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimewahi kusema wakati tunapitisha mipango yetu iliyopita kwamba Mheshimiwa Prof. Kitila anapenda majadiliano, ni mtu ambaye hachukii majadiliano

na hata baada ya kusoma mipango nilihamia mezani kwake pale, kuona kama hoja yangu anaweza kui-*withdraw,* lakini sikushawishika mezani kwa Mheshimiwa Prof. Kitila, kwa hiyo majadiliano yataendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma misingi ya mpango wetu, nikaona sentensi inayofariji sana inasema, msingi mkuu, imepambwa hivi hiyo lugha; "Msingi mkuu wa utekelezaji wa mipango yetu hii ni utawala bora, demokrasia, amani, pamoja na usalama." Kwa maoni yangu, ninaona maneno haya Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeamua kuwahadaa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivyo? Nimejaribu kusoma nyaraka hizi ili nione katika huu msingi mkuu kama kuna lolote ambalo limefanyika *so far.* Nimeenda kusoma taarifa ya utekelezaji, ninaona Mji wa Serikali Mtumba umejengwa, vituo jumuishi vya utoaji haki vimejengwa, na Mahakama imejengwa, nikastaajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mji wa Mtumba pamoja na kituo jumuishi ndiyo kinaleta demokrasia? Sijaona Katiba mpya, sijaona tume huru ya uchaguzi, sijaona utekelezaji wa ripoti ya haki jinai. Nikapata wasiwasi, nikasema labda Profesa anaona hakuna kilichofanyika, maana yake mimi ninaona…

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi. Ninataka tu nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, taarifa ambayo tunaizungumzia ya utekelezaji ni ya miezi mitatu; Julai, Septemba, na Oktoba. Mambo makubwa kama Katiba mpya, hutarajii yafanyike ndani ya miezi mitatu. Kwa hiyo, tuna Ilani ya miaka mitano mpaka 2030/2031, kwa hiyo atulie kazi inaendelea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ado, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ADO D. ADO: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa yake Profesa wangu kwa sababu msingi mkuu ungeanza kuonekana tangu mwanzoni. Ndiyo maana nikasema haya ni maneno matamu ya kuwahadaa Watanzania. Miezi mitatu tungeona *framework* japo ya kisheria, tungeona hatua yoyote japo kuelekea Katiba Mpya. Ukimya huu unamaanisha hata tutakapofika nusu mwaka katika robo ya pili, hali itaendelea kuwa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho tunalolijenga, ambalo nimelisema muda mrefu; Serikali ya Chama Cha Mapinduzi haina mpango wa kutuletea Katiba mpya, haitaki kuleta Tume Huru, haitaki kuweka mifumo mizuri ya kuleta haki jinai ndani ya nchi. Kama maneno haya yasingekuwa ya ukweli katika hii robo mwaka ya mwanzo, tungeona jambo lolote. Hilo nilitaka kulisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la tatu ni juu ya ajira. Tulikuwa na majadiliano mezani, sijaridhika. Takwimu zinazotolewa zinasema kwamba uhaba wa ajira, hali ya kukosa ajira imeshuka na takwimu za mwaka 2025 zinaonyesha kwamba imeshuka kutoka 6.2% mpaka kufikia 5.9%. Nikawa ninamhoji Profesa, wenzetu hizi ajira wanapata wapi? Mbona sisi tukienda huko vijijini, tunakuta vijana wamehitimu, yaani kila mwaka mgodi vyuo vikuu unatema vijijini, vijana wanarudi hawana ajira. Tunaona kwamba Serikali zile sekta ambazo zingeweza kuajiri vijana wengi; viwanda, sekta ya kilimo, sioni *visible transformations* ambazo zitani-*convince*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikawa ninamwambia Profesa, au tunapika *data* kujifurahisha? Sioni huku mtaani na ukizungumza na *Gen Z*, vijana watakwambia hakuna ajira. Tukienda kwenye makaratasi tunaambiwa hali ya ukosefu wa ajira imeshuka. Hili ni jambo ambalo tunapaswa tulichukulie kwa uzito kwa sababu hali ya kukosa ajira ni bomu linalosubiri kulipuka.

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha.

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa, ajiandae Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid.

MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Mpango wa Taifa na makadirio ya bajeti inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa mpango mzuri anaoufanya, alioupanga, lakini ninamshukuru na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta mpango huu katika Bunge ili tuweze kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote tunayoyapanga na kuyajadili ili yaweze kufanyika na kuweza kuitazama dira yetu, ni lazima nchi yetu iwe na amani. Bila amani, yote haya tunayoyaongea hayawezi kufanyika na mipango haiwezi kutimia. Pia, ni lazima tuwe na nguvu kazi. Ukisikia kuna mtu amepoteza uhai, ujue tunapoteza nguvu kazi na sisi tuwe wa kwanza kuhakikisha tunatetea na kudhibiti machafuko yoyote yanayoweza kutokea katika nchi yetu au katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo tutaweza kuhakikisha hii dira na kila kitu tunachokipanga kinaweza kufanyika kwa ufasaha na kwa utulivu. Pasipo amani hakuna maendeleo, pasipo amani hakuna maridhiano, pasipo amani hatuwezi kukaa hapa tukapanga chochote. Kwa hiyo, ninaomba tuzidi kuhimiza amani na utulivu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana mpango wetu unategemea vitu vitatu; Dira, Ilani na hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nimeandaa sehemu kama kumi hivi ambazo inabidi ziangaliwe na zitiliwe mkazo, japokuwa nitazifafanua kwa maeneo machache zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo inabidi yaangaliwe sana ili hii Dira iweze kutimia ni haya yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta muhimu ambazo lazima tuziangalie; kuna kilimo, mifugo na uvuvi; elimu na mafunzo; afya na huduma za jamii; miundombinu na usafirishaji; viwanda, biashara na uwekezaji; ajira kwa vijana na uwezeshaji wa wanawake; nishati, maji na mazingira; utalii na uchumi wa buluu; utawala bora na usimamizi wa fedha za umma; teknolojia, utafiti, na uchumi wa kidijitali. Tukiangalia haya mambo kumi na tukayaboresha na tukafanya kwa ufasaha, tutaweza kufikia dira yetu na mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na mipango. Kuna mipango ya kisekta, lakini kuna mipango ya kitaifa. Ninaishukuru Serikali imeweza kukamilisha mipango ya kitaifa. Kwa mfano, tumejenga Bwawa la Nyerere, huu ni mpango mkubwa wa kitaifa. Ujenzi wa *SGR*, ni mpango wa kitaifa. Tumejenga Daraja la Kigongo – Busisi, huu ni mpango wa kitaifa. Kwa hiyo, lazima tunavyokuwa na kipaumbele, vile vipaumbele ndiyo vitatupelekea sisi kuweza kufanya mpango wetu na dira yetu kuweza kukamilika kifasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kuna sehemu ambazo Serikali inabidi iwekeze. Sehemu hizo ni zile sehemu za uzalishaji. Unawekeza sehemu, unazalisha, halafu ndipo zile sekta nyingine zinawezeshwa kulingana na sehemu mlizowekeza. Hapa nimeainisha maeneo kama matano, sehemu ambazo inabidi Serikali kuwekeza: Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Viwanda, Utalii na Biashara. Mimi nitaongelea kilimo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo, inabidi sasa tuhame twende kwenye kilimo cha biashara. Kilimo cha biashara ni lazima tutengeneze miundombinu kwa wakulima. Kwa mfano, kila wilaya, kila kanda, kila mkoa una mazao yao ya kibiashara. Tujaribu kuwekeza sasa; kwa mfano, ukienda Rukwa, tuwe na mashamba makubwa Serikali iwekeze pale, tuweze kupata mashamba ya mahindi. Ukija Kagera pale, mashamba makubwa ya mibuni, lakini tuwe na kilimo cha umwagiliaji. Tukifanya haya

na kuwawezesha wakulima, kwa ardhi tuliyonayo na maji Mungu aliyotubariki, tutaweza kutimiza ahadi ya mpango wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifugo pia. Sisi kwetu tuna mifugo, tunalima. Tunawekezaje kwenye upande wa mifugo? Tunapata nini? Serikali inapata nini kwenye mifugo? Tujaribu kuwawezesha wafugaji kwa kutengeneza miundombinu bora ili waweze kufuga kwa ufasaha na inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huwezi kufanya yote haya kama hauna miundombinu. Miundombinu nimeigawa katika maeneo mawili. Hapa ninaomba nieleweke kidogo. Kuna miundombinu ambayo inaenda katika maeneo ya uwekezaji, kuna mashamba ya mahindi, lazima tuwe na barabara zinazoelekea kwenye maeneo ya mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kwetu kule kuna wafugaji wakubwa sana, ukienda Bugango, Bubale, ukienda Kikurura, watu wana mifugo. Serikali itengeneze barabara na miundombinu ya kwenda maeneo yale ili kupunguza gharama za usafirishaji. Kwa mfano, kwetu Bukoba Mjini tunakula ndizi kutoka Karagwe. Mtu anayetoka Murongo akisafiri kuja Bukoba ni kilometa 200. Barabara ikiwa ya lami, gharama ya ndizi Bukoba Mjini itapungua kuliko ilivyo sasa. Hiyo ni miundombinu inayoelekea katika maeneo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miundombinu ambayo nimeigawa katika kanda tisa, ambayo sasa vitu vikitoka kwenye maeneo ya uwekezaji mizigo iweze kusafirishwa kwenda nchi za jirani na kwingineko. Hii ninaomba niiweke vizuri ili waelewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ukanda wa *TANZAM (TANZAM Corridor)*; hii *TANZAM Corridor* ina kilometa 1,324. Hii inaanzia Dar es Salaam – Morogoro – Mikumi – Iringa – Mafinga – Mbeya – Tunduma. Ukanda huu pia unajumuisha na Barabara ya Mikumi – Ifakara – Mahenge – Mafinga – Mgororo, Mbeya – *Itungi Port*. Hizi barabara zikiimarishwa na zikajengwa kwa kiwango, zinaweza zikaongeza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukanda wa Kaskazini Mashariki *(North-Eastern Corridor)* wenye barabara urefu wa kilometa 955. Hii ni kuanzia Chalinze – Tanga – Moshi – Arusha – Himo – Marangu – Tarakea – Himo mpaka Holili kule kama unaenda Taveta, Kenya. Hapa kama tumelima mazao yetu tunaweza kuyasafirisha kuyapeleka Kenya na kuyapeleka nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo pia ukanda wa Kati *(Central Corridor)* wenye barabara za urefu wa kilometa 1,584. Hii inaanzia Morogoro – Dodoma – Mwanza hadi Rusumo, mpakani mwa Rwanda na Kobelo kama unaenda Burundi. Hapa unaweza ukasafirisha vitu vyote vinavyolimwa nchini na kuelekea maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ukanda wa Ziwa *(Lake Circuit Corridor)* wenye barabara yenye urefu wa kilometa 1,019. Hii ni kuanzia Sirari mpakani mwa Kenya, inakuja Musoma, inakwenda Mwanza, inakwenda Bukoba hadi Mutukula mpakani mwa Uganda. Hizi ndiyo barabara ambazo zikipewa kipaumbele zitaweza kuzalisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ukanda wa Kusini *(Southern Corridor)*. Hii inajumuisha barabara yenye urefu wa kilometa 1,024. Hii inaanzia Mtwara – Mingoyo – Masasi – Mang'aka – Tunduru hadi *Mbamba Bay* katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukanda wa barabara kuu za Kaskazini *(Great North Corridor)*, hii ina urefu wa kilometa 1,067. Iringa – Dodoma – Babati – Arusha hadi Namanga. Ukanda wa Magharibi, kilometa 1,286. Barabara hii inaanzia Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma hadi Nyakanazi. Halafu kuna ukanda wa Magharibi ambao una kilometa 1,021, Barabara hii inaanzia Mbeya – Rungwa – Ipole – Tabora hadi Nzega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunawezaje? Hizi kilometa zote ukiziangalia huwezi kuzitengeneza kwa siku moja, kihandisi. Sasa Serikali ije na kipaumbele kwa barabara hizi, kuwa miundombinu hii, inaenda kufanya nini? Kama tulivyofanya hii Miradi ya Bwawa la Nyerere na *SGR* ikawa mpango wa Taifa na hizi barabara

tunaweza kuziweka katika mpango wa kitaifa na siyo mpango wa Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiziangalia hizi barabara, tutaweza kuzalisha uchumi na hii inaitwa *Economical Corridor*. Tutaweza kuzalisha uchumi, bandari imefunguka, barabara zimetengenezwa. Tuweke kwenye mpango, ni barabara zipi zimeharibika sana na zinatengenezwa kwa kiwango gani, ili tuweze kufikia malengo ya dira yetu. Dhamira ya mpango huu ni kuhakikisha tunakuza uchumi wa wananchi na tunaongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufikia hayo ni lazima tuangalie katika nyanja hizi: Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Viwanda Na Utalii. Kwa mfano kwenye utalii, nchi nyingine zinafanya utalii kutokana na *population* ya watu. Tuna watu milioni 60, tukiweka utalii hapa Dodoma kuonyesha mila za Wagogo, chakula cha Wagogo, watu wa hapa Dodoma na sisi Wabunge tukalipa shilingi elfu moja moja kuangalia kwenye utalii ule wa hapa Dodoma, tutaongeza pato la Taifa. Dar es Salaam kuna watu wengi, kuna kituo gani pale kinachoweza kuleta watalii na kuingiza pesa? Tuhame kwenye utalii wa kwenda kuangalia mbuga za wanyama, lakini tuangalie na utalii wa asili tena ambao unalinda na utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote, takwimu zote zilizotolewa, takwimu zote walizozitoa; zile nchi ziliwekeza, maeneo yale na ndiyo takwimu zikazaliwa. Ukisikia China uchumi wao umepanda, ukisikia China wanazalisha, lazima kwanza walizalisha. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali tuweze kuwekeza kwenye taasisi, kwenye hizi sekta za uzalishaji, ili tuweze kuongeza uchumi wetu na zile taasisi nyingine zitegemee uzalishaji ambao tutakuwa tunaufanya sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushukuru kwa kupewa nafasi ya kuchangia katika mpango huu mzuri, twende kwenye utekelezaji sasa. Mpango bila utekelezaji unakuwa siyo mpango tena. Ahsante kwa kunipa nafasi hii.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, ajiandae Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima.

MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na wenzangu waliotangulia kwa kutoa pongezi kwa Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Naibu Waziri, watendaji wote wa Wizara hii. Pia, ninampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Wajumbe wake wote kwa kazi nzuri ambayo wametuletea kwenye huu ukumbi wetu, kiasi cha kwamba tunapata nafasi na sisi kuweza kutoa maoni yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika, Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume alisema; "Mipango bila fedha ni sawa na mipango hiyo kuwa ni rasimu tu." Moja ya eneo ambalo tumekuwa na changamoto nalo kwa muda mrefu sana ni *deficit budget,* kwamba tumekuwa na mipango mizuri sana, lakini kutokana na changamoto ya fedha hatua za utekelezaji zinasababisha mipango hiyo kushindwa kutekelezeka kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachokuwa kinaendelea ni *carry forward*, ile mipango ambayo tumepanga na tumeshindwa kuitekeleza katika mwaka wa fedha 2026/2027, inatulazimu twende nayo katika mwaka wa fedha 2027/2028. Kwa hiyo, ni mchakato ambao tutakuwa tunaendelea nao kila siku. Wapo wenzangu ambao wamechangia hapa asubuhi ya leo na moja ya jambo ambalo walikuja nalo ni kuona kwa namna gani tunapata suluhisho la namna ambavyo tunaweza kufanikisha miradi yetu hii ambayo tumeipanga katika mwaka wa fedha husika wa 2027/2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya wazo ambalo nimekuja nalo kwa Serikali, ni kufikiria kuanzisha kitengo cha *Project Finance*. Kitengo ambacho kitakuwa na jukumu ambalo haliambatani moja kwa moja na *PPP*. Japokuwa ipo mifano mbalimbali ya wenzetu ambao wana kitengo cha *PPP* na ndani yake kuna kitengo cha *Project Finance,* lakini kwa mazingira yetu sisi na kwa *speed* ambayo tunatarajia kuweza kufikia 2050, ni lazima tuwe na vitengo viwili tofauti. Kitengo cha *PPP* kiendelee kuratibu miradi ya *PPP*, lakini pia tuwe na kitengo mahususi ambacho kitahusika na hizi *Project Finance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio ni kwamba tukiwa na kitengo hicho, kitaweza kufanya kazi zifuatazo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kwanza, itaweza kutambua miradi ambayo inaweza kufadhiliwa kwa njia hiyo mbadala kama *Project Finance*. Pia, kitengo hiki kitaweza kufanya tathmini ya uwezo wa mradi kujilipia. Katika mazingira haya unaweza ukaona, baadhi ya taasisi wanaweza kuwa na mradi ambao unajikidhi kabisa kukopa fedha, kufanya uwekezaji na kufanya *return* kutokana na mradi ule, lakini tu kwa sababu ya *balance sheet*, inapelekea kukosa mkopo wa aina ile. Kwa hiyo, tutakapokuwa na kitengo ambacho tumekipatia hii kazi, kitakuwa kinaweza kufanya tathmini ya miradi hiyo na kutoa miongozo kwa namna ambayo fedha itapatikana ambayo itasaidia katika utekelezaji wa mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu lingine la hiki kitengo ni kuandaa mikakati ya ufadhili juu ya miradi. Tuweze kuainisha miradi gani ambayo itakuwa ni ya kimkakati. Namna ambavyo tutasimama kwa pamoja kuweza kuzipatia fedha ili kutekeleza miradi hiyo. Kitengo hicho twende tukakipe jukumu lingine la kutafuta wawekezaji na wakopeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, kitengo hicho twende tukakipatie kazi ya kufuatilia utekelezaji wa ufadhili na mwisho kabisa, kitengo hicho tutakipa kazi ya kutathmini matokeo baada ya mradi kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuwa na kitengo cha aina hiyo na tukaweza kukipatia majukumu hayo, tunatarajia kupata faida zifuatazo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tutaweza kupunguza utegemezi wa bajeti ya Serikali. Wabunge wengi wamekuwa wakichangia na jana wakati wa maswali, moja ya eneo ambalo limekuwa lina mahitaji makubwa sana ni juu ya miradi yetu ya barabara. Unaweza ukaona, licha ya mipango mizuri ambayo Serikali inafikiria na licha ya fedha ambazo wanazipeleka kwenye miradi hiyo, lakini utekelezaji wake bado unaonekana haujaakisi shauku za Wabunge wengi. Kama tutaweza kufanikisha hayo, tunatarajia fedha ambayo imebakia ya Serikali tutaweza kupeleka katika miradi mingine na tutaweza kupunguzia mzigo Serikali yetu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine ambayo tunaweza kuipata ni kuongeza uwezo wa kutekeleza miradi mikubwa ambayo tunaweza kuwa nayo. Katika hili ninaendelea kumpongeza sana Waziri wa Maji; kupitia Mfuko wa Maji wamekuja na wazo zuri sana ambapo kwa zile taasisi za maji ambazo zinajiweza, wamekuwa wakizisimamia ziweze kupata fedha hizi ili kuwekeza, mwisho wa siku zimeweza kuendelea kutoa huduma na kuwa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine, tutaweza kuimarisha tathmini ya uwekezaji. Mwisho kabisa, moja ya dhamira kubwa ya Serikali ni kuongeza uwajibikaji na tija. Wananchi wetu wanatarajia kuweza kupata tija ambayo itatokana na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ninataka kuzungumzia ukiacha hili la Kitengo cha *Project Finance* ni suala zima la mfumo wa *e-delivery*. Moja ya eneo muhimu sana ni suala la ufuatiliaji na tathmini. Tumekuwa na mipango mizuri sana, lakini bila kufanya ufuatiliaji na tathmini inawezekana tukashindwa kujijua wapi tulipo na wapi tunaelekea. Moja ya dhamira kubwa sana ya ufuatiliaji na tathmini ni kuona *relevance* ya mradi, kuona

outcome ya mradi, kupata *efficiency* ya mradi, lakini mwisho wa siku kuweza kupatikana tija ambayo inatarajiwa katika mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Tume ya Mipango ya tarehe 5 Septemba, 2026, kati ya miradi 500 ambayo tulitarajia kuweza kuisajili kwenye mfumo wetu wa *e-delivery*, ni miradi 150 tu ambayo imeweza kusajiliwa. Unaweza ukajenga picha kwamba kazi ya ufanisi ya ufuatiliaji hatuwezi kuifikia. Katika hili nilikuwa nina ushauri ufuatao:

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kufanya uhakiki wa kitaifa juu ya miradi yetu yote. Hii ambayo imebakia, ambayo hatujaingiza lakini na hiyo ambayo tunatarajia kuja kuiingiza katika mwaka wa fedha 2027/2028. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kutoa taarifa za utendaji. Kuweza kupata ripoti kwa kila kipindi cha *quarterly*. Hii itaweza kutuongoza, wapi tulipo, wapi tumefikia, lakini wapi tuweze kuongeza nguvu. Inawezekana tusisubiri matokeo ya mwisho, wakati wa *activities* zenyewe zikawepo kasoro ambazo zinaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kupima matokeo. Ni lazima ufike wakati kwamba mfumo huu uwe rafiki na uendane na uhalisia wa kupata matokeo ambayo tunayatarajia kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, kwenye huu mfumo kuwepo na mfumo wa alama ambao tunatarajia utaweza kuzingatia *Project Performance Scorecard*. Haya ni maoni yangu, ambayo ninatarajia kwamba tukiweza kuyaboresha kwenye huo mfumo wetu wa *e-delivery* ni matarajio yetu kwamba ufanisi wa kazi zetu ambazo tumezipanga, tutaweza kuufikia kama ambavyo tulitarajia na mwisho wa siku, matarajio ya Serikali yetu ya utekelezaji wa mipango yetu tutaweza kuyafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima.

MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii adhimu ya kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Leo hii nitajielekeza kwenye Sekta ya Kilimo. Katika Sekta ya Kilimo nitafungamanisha na mapinduzi ya viwanda na biashara. Katika Sekta ya Kilimo, mimi leo nitazungumzia zao la tumbaku. Nitaangalia jinsi Serikali inavyoweza kusaidia kuwekeza katika taasisi za utafiti kama *TARI-TORITA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wote tunavyofahamu zao la tumbaku kwa sasa ni zao la pili ambalo linaongoza kuleta pesa za kigeni, ikianza na korosho. Sasa *TARI-TORITA* kama mtafiti wa zao hili, bajeti yake na miundombinu ya kimaabara siyo mizuri. Tunavyoelekea katika Dira ya Mwaka 2050 ninaomba kuongelea mambo machache ambayo yanaweza yakatusaidia katika kufanya mapinduzi katika zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa takwimu mwaka 2020 zao hili la tumbaku tulizalisha kilo 42,000, lakini kufika mwaka 2024/2025 tumezalisha zaidi ya kilo 185,000,000 ambazo ni sawa na thamani ya dola milioni 475.5. Kwa hiyo, utaona ni jinsi gani tumepiga hatua kubwa sana katika zao hili. Bado tuna changamoto kubwa sana katika zao hili ambalo linatufanya tusifikie malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Zimbabwe mwaka 2024/2025, wenzetu wameweza kuzalisha zaidi ya kilo milioni 355. Suala hili kama Zimbabwe wanaweza ni kwamba hata sisi Tanzania tunaweza kwa sababu uwezo huo tunao. Sasa *TARI-TORITA* kama Taasisi ya Utafiti bado tuna maabara za kizamani ambazo miundombinu yake ni ya kizamani, lakini bado bajeti yake ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Taasisi kama *TARI-TORITA* ikiwezeshwa kimiundombinu na kibajeti nini tunaweza kufanya?

Kwanza, tunaweza kupunguza *cost of production, k*wa sababu kwa sasa hivi suala ambalo tunalipata katika zao la tumbaku ni kuwa na *cost of production* ambayo ni kubwa sana. Ukiangalia sisi kama Tanzania mwaka jana kwa mbolea tu, mpaka imemfikia mkulima ni zaidi ya dola 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Zimbabwe, Zambia wenzetu wamepata mbolea *almost* kama dola 35. Wenzetu ukija kwenye uzalishaji, wanazalisha mpaka heka kwa kilo 1,200 mpaka 1,700, lakini sisi ukiona mtu kazalisha sana kwa heka anaenda mpaka kilo 700 tu. Kwa hiyo, *cost of production* ziko juu sana. Siyo hivyo tu, tunabidi tuwekeze katika maabara hizi ili tuweze kupata mbegu ambazo zitaongeza mavuno na siyo kuongeza mavuno tu, mbegu ambazo zitakuwa zina ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto mojawapo tunayoipata sasa hivi ni kuwa na mbegu za tumbaku ambazo hazina ubora na hazikidhi mahitaji ya wanunuzi. Pia, kama mnavyofahamu, zao hili linauzwa katika nchi za nje na wanunuzi wakubwa kama Philip Morris na wengineo wana vigezo vyao wanavyovihitaji. Sasa hivi wamekuja na *conditions* nyingi sana wanavyonunua zao hili. Tusipo-*meet conditions* za hawa wanunuzi itafika mahali zao hili tutashindwa kuliuza na kupata mapato yale ambayo tunayategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba kushauri kuwekeza katika utafiti wa mbegu. *TARI-TORITA* sasa hivi wamejikita sana kufanya utafiti katika kuja na mbadala wa mbolea, matumizi sahihi ya mbolea, lakini pia kupunguza kutumia mbolea zenye kemikali. Sasa maabara zetu zinakosa kufanya uchunguzi wa *chemical analysis* ambayo itakidhi *industrial preference*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema awali, wanunuzi wengi wa tumbaku wana *conditions* zao. Ukienda China utakuta wanataka tumbaku ambayo *sugar* iko juu, ukienda nchi nyingine wanataka tumbaku ambayo *nicotine* iko juu. Sasa kutokana na kwamba hatuna mbegu bora ambazo hazikidhi soko la zao hili inafika kipindi, maana yake hata tumbaku yetu tunaiuza kwa bei ya chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi pia tuwekeze katika utafiti. Kama *TARI-TORITA* wanaweza wakapata bajeti inayotosha, wanaweza wakafanya utafiti ambao utaenda moja kwa moja kwa mkulima na hii itasaidia utafiti huu ukalenga mazingira. Mtu wa Chunya akafanyiwa utafiti kutokana na mazingira ya Chunya na mtu wa Kaliua akafanyiwa utafiti kutokana na mazingira ya Kaliua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARI-TORITA* kutokana na ufinyu wa bajeti, wanafanya utafiti jumuishi. Siku ya mwisho utafiti huu ukimfikia mkulima unakuta haukidhi mazingira husika. Kwa hiyo, kama wakiongezewa bajeti, wana uwezo wa kupanua wigo wa kufanya utafiti kwa kumfikia mkulima moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatakiwa pia kuwekeza katika utafiti wa mbegu ambazo ni *hybrid*. Kwa sasa hivi mbegu tunazozitumia zinatoka nje, lakini hizi mbegu tunaweza tukafanya utafiti na tukazitengeneza hapa hapa nchini. Hilo jambo linawezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kubuni teknolojia na vifaa vizuri vinavyoweza kutengeneza mbegu. *TARI-TORITA* kwa sasa kama nilivyosema, tuna shida katika uwekezaji wa mbolea na vitalu, kwa sababu hatuna teknolojia zinazokidhi hitaji hili. Ukienda kwa watu ambao wanafanya *horticulture*, utaona kabisa wenzetu wamepiga hatua. Kwa hiyo, ninajua tuna uwezo wa kutohoa mbinu ambazo wanazifanya upande wa *horticulture* tukaja tukazi-*practice* kwenye zao la tumbaku na tukafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji waliotangulia wengi wameeleza kuhusu *PPP*. Ninajua kabisa Sekta ya Kilimo, (Wizara ya Kilimo), tuna wanunuzi wakubwa sana wa tumbaku, ambao wana uwezo wa kukaa nao chini, wakafanya maandiko ambayo yana tija, wakaweza kuja kuwekeza katika hizi maabara kwa sababu, wanunuzi wakubwa wa tumbaku wanataka tumbaku iliyo bora. Kwa hiyo, ninajua tukifanya maandiko ambayo yana tija hawatashindwa kuja kuwekeza kwenye maabara hizi ili tuweze kupata tumbaku yenye ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa ninaendelea kumalizia, ninapenda kuipongeza Serikali yetu. Nilishawahi kusimama katika Bunge hili na nikaliomba Bunge hili na Serikali yetu Tukufu tuweze kuongeza wigo wa wanunuzi wa tumbaku. Nimeona kuna hatua kubwa sana zinapigwa na sasa hivi tumeona Serikali yetu imeanza kuingia makubaliano na wanunuzi wa tumbaku kutoka China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii inaonesha kabisa tuna tija kubwa ya kuwekeza katika sekta ya tumbaku kwa sababu tunatakiwa kukidhi mahitaji ya wanunuzi kwa sababu uhitaji wa tumbaku unaenda kuwa mkubwa. Uhitaji wa tumbaku ukienda kuwa mkubwa, hatuwezi kukidhi kama hatujawekeza kwenye utafiti wa zao hili ukijumlisha kupunguza *cost of production*, lakini kuwekeza kwenye mbolea bora na mbegu iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja mchangiaji wetu wa mwisho siku ya leo atakuwa ni Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima.

MHE. DKT. REGINA C. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia Mpango wetu wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2027/2028. Kwanza kabisa, niipongeze Serikali yetu kwa kuendelea kuona namna bora ya kuendelea kuunganisha mipango hii ya maendeleo na Dira ya Mwaka 2050. Nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na timu yake. Ameendelea kutoa dira na namna ambavyo Taifa letu linapaswa kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, kuna mambo machache ambayo nitayaongea hapa ikiwemo pamoja na kupongeza namna ambavyo mipango hii ina mahusiano na Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050. Tumeona pia kuna viashiria vya mpango, takribani viashiria 305 ambavyo viko katika mpango huu. Hili ni jambo la msingi sana, tunapokuwa na hizi *key performance indicators* zinatoa mwelekeo na namna ambavyo

yale yaliyopangwa yanaenda kuonekana kama *output* kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia huu mfumo wa *e-delivery* wengi wameuelezea hapa, ni mfumo mzuri ambao utasaidia masuala ya ufuatiliaji katika utekelezaji wa miradi yetu mbalimbali. Hili ni jambo ambalo linaenda kuonesha uwazi, ufuatiliaji na uwajibikaji. Kwa maana hiyo, niendelee kupongeza mpango huu na namna ambavyo imeendelea kuonesha mipango hii inavyopaswa kuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kama wawakilishi wa wananchi na wengine ni wawakilishi wa makundi maalum, wajibu wetu mkuu siyo kuona mpango huu unapangwa namna gani. Kikubwa tunachopaswa kuona ni namna mabadiliko yanakwenda kuonekana kwa wananchi wetu ambao tunawaongoza. Hilo ndiyo kubwa ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wanatamani kuliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huu, nitakuwa nina jambo moja tu ambalo ninataka niliongee katika mpango huu. Tumeona kabisa mpango huu unaenda kuwa tegemezi kwa asilimia kubwa katika sekta binafsi. Kwa maana ya takribani 62.31% inaenda kutegemezwa katika kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si jambo baya, lakini kwa mujibu wa taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki ya Dunia, sekta binafsi ina fursa ya kukua, lakini bado inakabiliwa na changamoto nyingi sana. Takwimu katika Benki ya Dunia na hii Ofisi ya Takwimu, inaonesha kabisa kwamba, siyo tayari Sekta hii imekua, inategemea kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa niombe tu nitoe angalizo kwamba tunapaswa kuangalia namna gani Sekta hii italeta tija katika ku-*support* mpango huu. Tunahitaji Sekta hii ikionekana kupanuka wakati ina-*support* mpango wetu wa maendeleo, lakini pia kuongeza uzalishaji na kutengeneza ajira bora, jambo ambalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto nyingi sana. Ninamshukuru Profesa Muhongo alitoa takwimu nzuri tu hapa, lakini bado kwenye sekta hii isiyo rasmi kuna changamoto. Hii Sekta ni pana, inaweza ikawa ni katika sekta kubwa, sekta za kati na hizi ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaona kuna changamoto kubwa sana. Upatikanaji wa mitaji na mikopo nafuu kwa watu wetu bado ni changamoto. Pia, takwimu zinaonesha kabisa, kwa *research* ambazo zimefanyika, takribani 48% ya watu ambao wamekuwa wanafanya kazi katika sekta hii, bado wana changamoto ya kupata mikopo nafuu na mitaji kutoka katika taasisi zetu za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kuona tozo na urasimu usiokuwa na tija. Hili kama Profesa unataka hii sekta iweze kuwa na mchango mkubwa ni lazima haya maeneo kuyaangalia kwa kina. Hizi tozo na urasimu ambazo zimeendelea kuonekana, basi ziweze kushughulikiwa na watu wetu waweze kufanya shughuli kwenye tija na waweze kuchangia mpango huu katika masuala ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna gharama za uendeshaji, masuala ya umeme. Kwa takwimu ambazo zimefanyika, 71.8% ya watu ambao wako kwenye sekta hii binafsi bado wanakabiliwa na changamoto za umeme. Kwa maana hiyo, wamekuwa na changamoto kubwa katika kutekeleza shughuli zao katika tija inayotakikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiangalia yote haya, bado kuna jambo ambalo Serikali inapaswa kulifanya katika Sekta hii binafsi ili iweze kweli kuchangia mpango huu katika kutekeleza. Nini kifanyike sasa? Ninayo mambo machache ambayo ninashauri. Tumeona kilimo na uvuvi ni eneo ambalo lina wigo mpana wa kusaidia utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali iweze kuliangalia hili kwa upana wake namna ya kuboresha kilimo chetu, kwa sababu ukifanya tathmini ya kina, bado kuna changamoto

kubwa sana katika kilimo na hata masuala ya ufugaji. Pamoja na kwamba Serikali imeendelea kuweka hatua mbalimbali za ku-*promote* kilimo, lakini bado tuna mambo mengi ya kufanya hapa. Pia, hii ya kupunguza tozo na urasimu kwenye taasisi zetu ambazo zinasaidia utekelezaji wa majukumu mbalimbali wa sekta hii isiyo rasmi au sekta binafsi, basi viweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwezesha upatikanaji wa mitaji nafuu. Waheshimiwa Wabunge wengi nina imani kabisa wanapokuwa katika majimbo yao, suala la upatikanaji wa mitaji bado ni changamoto kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, niombe tu, Mheshimiwa Profesa anapoangalia Sekta hii kuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa mpango huu, lazima aangalie namna ya upatikanaji wa mitaji nafuu kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhakikisha upatikanaji wa nishati na miundombinu ya uhakika. Bado tuna changamoto kubwa sana katika sekta binafsi na namna ambavyo nishati na miundombinu ya uhakika inavyoweza kupatikana. Barabara zetu bado ni changamoto, masuala ya umeme, masuala ya maji bado tumeendelea kuona yakiwa yana changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nina imani kabisa lengo la Serikali yetu ni jema sana. Tunatamani kuona Sekta hii ikiboreshwa ili iweze kuchangia utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako na huyo ndiye alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

Ninaomba nimtambulishe mgeni wa Mheshimiwa Ibrahim Shayo ambaye ni Ndugu Alfred Andulea ambaye ni msanii maarufu pale Moshi akijulikana kama K Sali Tena. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge ninaomba kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 6.38 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 30 Oktoba, 2026 Saa Tatu Asubuhi)

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA